

**UCHAMBUZI LINGANISHI WA MAUDHUI NA MAJUKUMU YA NYIMBO ZA  
HARUSI ZA WADIGO NA WASWAHILI.**

**MARIAM DAU NGOME**

**C50/75723/2012**

**WASIMAMIZI**

**PROF. KINEENE WA MUTISO**

**PROF. RAYYA TIMAMMY**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU  
CHA NAIROBI.**

**NOVEMBA 2014**

## **IKIRARI**

Tasnifu hii ni matokeo ya juhudi za utafiti na si kazi ya mtu mwingine. Kazi hii haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

### **Mtahiniwa**

**Sahihi.....**

**Tarehe.....**

**Mariam Dau Ngome**

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

**Sahihi.....**

**Tarehe.....**

**Prof. Kineene wa Mutiso**

**(Msimamizi)**

**Sahihi.....**

**Tarehe.....**

**Prof. Rayya Timammy**

**(Msimamizi)**

## **TABARUKU**

Kazi hii ninamtabarukia mamangu mpendwa Mejumaa Saidi kwa juhudi zake za kunilea, kunielimisha, kunifunza haja ya uvumilivu maishani, kunishauri na kuniunga mkono kwa lolote nililoazimia kufanya.

## SHUKRANI

Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kukamilisha kazi hii. Kisha, shukrani zangu zisizo na kifani zimwendee msimamizi wangu Prof. Kineene wa Mutiso kwa mawaidha na ushauri wake wa busara, mwongozo na masahihisho aliyonipa wakati nilipokuwa na matatizo ya kutofahamu njia ambayo ningefuata katika hali hii ya usomi na utafiti, Nampa hongera kwa namna alivyopitia sehemu mbalimbali za kazi yangu kwa makini na kuniwezesha kuukamilisha utafiti wangu kwa muda unaofaa.

Shukrani pia nazitoa kwa Prof. Rayya, ambaye hakuchoka kusoma kazi yangu mara kwa mara. Uhakiki wake pamoja na maoni yake ndiyo yaliyoupatia utafiti huu sura iliyo nayo. Kwa masahihisho na mawaidha yake, namshukuru na kumwomba Mola azidi kumpa maarifa na neema. Mbali na wasimamizi wangu, niliweza kupata ushauri wa kitaalamu na kiusomi kutoka kwa wahadhiri mbalimbali katika idara ya Isimu na Lugha katika Chuo kikuu cha Nairobi. Nawapa Shukrani kwa kazi bora ya mwongozo walionipa katika harakati yangu ya kusomea shahada ya uzamili. Miongoni mwao ni Prof. John Habwe, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Jefa Mweri na Dkt. Amir Swalehe. Ustadi wenu ndio ulionipa hamu ya kutaka kuendelea tena na tena.

Aidha, nawashukuru wenzangu ambao tulikuwa pamoja nao katika safari hii ya usomi wa shahada ya uzamili. Hawa ni Furaha, Jael, Jane na Ruth. Mijadala kadha tulioshiriki na ushirikiano ulisaidia kurahisisha mambo yalipoonekana magumu.

Sitasahau marafiki zangu na dadangu Nzadze kwa kunipa usaidizi wa hali na mali, wakati wa masomo yangu hasa katika kipindi kigumu cha utafiti.

Heko na shukrani nawatunukia mume wangu, Karissa Charo, watoto Juma, Ali na Salma kwa kuvumilia. Ningependa kumshukuru mama yangu Bi. Mejumaa kwa kuvumilia maisha magumu nilipokuwa nikiendelea na masomo yangu. Pia, ninashukuru Chuo kikuu cha Nairobi kwa kuniamini na kunipa fursa ya kuendelea na masomo yangu ya shahada ya uzamili kikamilifu.

Mwisho, ninawatolea shukrani wale wote waliojitolea kupiga chapa tasnifu hii. Shukrani kwenu nyote ambao nimewataja na wale sijawataja, ninawatakia kila la heri maishani.

## **IKISIRI**

Utafiti huu unahusu uchambuzi linganishi wa maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Kazi hii imegawanywa katika sura nne. Katika sura ya kwanza tumeangazia maswala muhimu ya utafiti wetu. Tumeelezea swala la utafiti, madhumuni na nadharia tete zilizotuongoza. Aidha, sababu za utafiti zimeelezwa pamoja na upeo na mipaka. Msingi wa nadharia wa utafiti umefafanuliwa na yaliyoandikwa kuhusu mada yalijadiliwa. Mwisho, mbinu za utafiti zimebainishwa na uchanganuzi wa data umefanywa. Katika sura ya pili, tumeshughulikia utaratibu wa ndoa na harusi za Wadigo na Waswahili. Aidha, katika sura ya tatu tumeangazia maudhui na majukumu katika nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Mbali na haya, pia tumeshughulikia walengwa wa ujumbe katika nyimbo hizi. Mbali na hayo, tumelinganisha na kutofautisha maudhui na majukumu yanayojitokeza katika nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Sura ya nne, ambayo ndio ya mwisho, tumejikita katika matokeo ya utafiti, changamoto tulizokumbana nazo na pia tumetoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye kuhusu mada hii.

## YALIYOMO

Ikirari.....	ii
Tabaruku .....	iii
Shukrani .....	iv
Ikisiri.....	vi
Yaliyomo.....	vii
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
1.0 UTANGULIZI .....	1
1.1 Tatizo La Utafiti.....	2
1.2 Madhumuni Ya Utafiti.....	3
1.3 Nadharia Tete.....	4
1.4 Sababu Za Kuchagua Mada .....	4
1.5 Upeo Na Mipaka.....	5
1.6 Msingi Wa Kinadharia Wa Utafiti.....	6
1.7 Yalioandikwa Kuhusu Mada.....	8
1.8 Mbinu Za Utafiti .....	9
1.9 Hitimisho.....	10
<b>SURA YA PILI:HARUSI NA NDOA .....</b>	<b>11</b>
2.0 UTANGULIZI .....	11
2.1 Utaratibu Wa Harusi Na Ndoa Za Wadigo Wa Tiwi.....	11
2.1.1 Posa.....	12
2.1.2 Kupeleka mizigo .....	16
2.1.3 Matayarisho ya harusi .....	21
2.1.4 Harusi.....	22
2.2 Utaratibu Wa Harusi Na Ndoa Za Waswahili Wa Lamu.....	27
2.2.1 Posa.....	27
2.2.2 Kupeleka mahari .....	28
2.2.3 Harusi.....	30
2.3 Hitimisho.....	33
<b>SURA YA TATU:NYIMBO ZA HARUSI .....</b>	<b>34</b>
3.0 UTANGULIZI .....	34

3.1 Nyimbo Za Kiasili.....	34
3.1.1 Nyimbo za harusi za Wadigo.....	34
3.1.2 Maudhui.....	35
3.1.3 Maombi.....	35
3.1.4 Umuhimu wa kuowa mbali.....	36
3.1.5 Msamaha.....	36
3.1.6 Uvivu.....	37
3.1.7 Ukosefu wa wajibikaji.....	38
3.1.8 Majukumu ya bwana.....	38
3.1.9 Wivu.....	39
3.1.10 Ushirikina.....	41
3.1.11 Umbeya.....	41
3.1.12 Tamaa na ubinafsi.....	42
3.1.13 Umoja na ushirikiano.....	43
3.2 Majukumu.....	44
3.2.1 Kuhifadhi.....	45
3.2.2 Kuhimiza.....	46
3.2.3 Kukashifu.....	47
3.2.4 Kuhamasisha.....	48
3.3 Walengwa Wa Ujumbe.....	49
3.4 Nyimbo Za Harusi Za Waswahili.....	49
3.4.1 Maudhui.....	49
3.4.1.1 Maombi.....	49
3.4.2 Mapenzi.....	50
3.4.3 Unafiki.....	51
3.4.4 Vijembe.....	51
3.4.5 Pongezi/Kusifu.....	52
3.4.6 Majuto.....	52
3.4.7 Majukumu Ya Bwana.....	53
3.4.8 Mapishi.....	53
3.4.9 Uasherati.....	54



3.4.10 Madhara Ya Kupenda .....	55
3.5 Majukumu .....	55
3.5.1 Kuhimiza.....	56
3.5.2 Kuhamasisha .....	56
3.5.3 Kuelimisha .....	57
3.5.4 Kukejeli.....	57
3.5.5 Kuhifadhi Utamaduni.....	58
3.5.6 Kuzindua .....	58
3.6 Walengwa Wa Ujumbe .....	59
3.7 Taarab .....	59
3.7.1 Maudhui .....	60
3.7.1.1 Ukosefu wa imani.....	60
3.7.1.2 Kupeana tahadhari .....	60
3.7.1.3 Kutolipiza kisasi .....	61
3.7.1.4 Masuala ya Dini.....	61
3.7.1.5 Uvumilivu.....	62
3.7.1.6 Malezi .....	62
3.7.1.7 Mapenzi .....	63
3.7.1.8 Maombi .....	64
3.7.1.9 Maadili katika ndoa.....	64
3.8 Majukumu .....	65
3.8.1 Kuhimiza.....	65
3.8.2 Huelimisha .....	65
3.8.3 Huzindua .....	66
3.8.4 Kukashifu .....	66
3.9 Walengwa .....	66
3.10 Kulingana Kimaudhui Baina Ya Nyimbo Za Kiasili Za Harusi Za Wadigo Na Waswahili.	66
3.11 Kutofautiana Kimaudhui Katika Nyimbo Za Asili Za Harusi Za Wadigo Na Waswahili ...	67
3.12 Ulinganishi wa kimajukumu baina ya nyimbo za kiasili za harusi za wadigo na waswahili.	69
.....	69
3.13 Hitimisho.....	71

<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>71</b>
4.0 UTANGULIZI .....	72
4.1 Upimaji Wa Madhumuni .....	73
4.2 Upimaji Wa Nadharia Tete .....	73
4.3 Changamoto Za Utafiti .....	74
4.4 Mapendekezo .....	75
MAREJELEO .....	76
KIAMBATANISHO I:Baadhi Ya Wahojiwa.....	79
KIAMBATANISHO II:Nyimbo Za Harusi .....	81

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Wadigo ni kabila mojawapo ya makabila tisa yanayounda kundi la Wamijikenda. Kulingana na Spear (1978), asili ya Wamijikenda ni Shungwaya, katika bonde la Mto Juba. Wadigo walikuwa wa kwanza kushambuliwa na Wagalla, hali iliyowafanya waondoke kuelekea pwani hadi Shimba Hills, Kusini Magharibi mwa Mombasa ambapo walianzisha kaya Kwale. Baadhi ya Wadigo kutoka kaya Kwale waliondoka na kwenda kuanzisha kaya Kinondo.

Vikundi vidogo vidogo kutoka kaya hizi mbili vilianza kuondoka na kwenda kudumisha kaya zingine ndogondogo. Kwa mujibu wa Spear, Mijikenda ni wakulima na wafugaji tangu walipokuwa Shungwaya. Mbali na kilimo walijihusisha na biashara, walifanya biashara na Waswahili

Shughuli ya biashara baina ya Wadigo na Waswahili ilisababisha mwingiliano kati ya jamii hizi mbili. Baada ya Wadigo kudumisha makao katika kaya Kwale na Kinondo walikuwa majirani wa Waswahili. Ujirani ambao umesababisha mwingiliano wa kila namna, hali inayoleta utata katika kuweka mpaka baina ya Udigo na Uswahili.

Mbali na ujirani, jambo lingine linalosababisha hali hii ni kwamba, makundi haya mawili ni wafuasi wa dini ya kiislamu. Wameingia katika Uislamu na wakakubali utamaduni wake hali ya kwamba utamaduni wao wa kiasili yaani Wadigo na Waswahili unafifia. Hali hii inadhihirika kupitia mavazi, salamu, shughuli za mazishi, kutoa jina kwa mtoto na shughuli za harusi.

Wanawake wavaa mabuibui au kujitanda lesa mbili nao wanaume huvaa kanzu na kofia au kikoi na fulana. Salamu zinazotumiwa watu wawili wanapokutana ni zile za kiislamu yaani “Asalaam alaikum” na majibu yake ni, “Waaleikum Salaam.”

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), nyimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimuziki au wizani. Nyimbo huchukua sehemu kubwa katika miviga ya jamii mbalimbali. Harusi ni sherehe inayoandaliwa wakati wawili wanapooana. Pia harusi katika jamii ya Wadigo humaanisha utaratibu mzima wa kufungishwa kwa nikaha. Kuna shughuli mbalimbali ambazo ni lazima zitekelezwe.

Shughuli hizi hujumuisha pande zote mbili za maharusi, jamii ya bwana harusi na jamii ya bibi harusi. Katika sherehe za harusi huwa na nyimbo. Mara nyingi nyimbo hizi huimbwa na wanawake. Sio kwamba wanaume wanakatazwa, lakini utapata wanawake ndio hujishughulisha na kuimba. Ni nadra sana kuwapata wanaume wakiimba katika sherehe hizi. Wakati mwingine nyimbo za harusi huambatana na ala kama vile ngoma. Utaratibu wa harusi huwa na hatua mbalimbali na kila hatua huwa na shughuli zake ambazo ni tofauti na za hatua nyingine. Hatua zote kwa jumla na shughuli zinazoendeshwa huchangia ufanisi wa shughuli nzima ya harusi. Shughuli za kila hatua huambatana na nyimbo. Hali hii husababisha uainishaji wa nyimbo za harusi katika makundi tofauti tofauti. Maudhui ya nyimbo za harusi hutofautiana, kulingana na shughuli zinazoendeshwa katika hatua hiyo ya shughuli za harusi. Kwa kuwa nyimbo hizi huwa na mawazo mazito na hupaniwa kuonyesha uhusiano wa kijamii, kukejeli, kuburudisha na kadhalika, hali hii ndio iliyopelekea haja ya kufanywa kwa utafiti wa maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi katika jamii ya Wadigo na Waswahili.

### **1.1 Tatizo La Utafiti**

Harusi na ndoa ni shughuli muhimu sana katika jamii ya Wadigo na Waswahili. Sherehe hii huambatana na nyimbo na hata wakati mwingine muziki kama vile taarab huchezwa.

Nyimbo hizi huimbwa ili kuburudisha hadhira. Mbali na kuburudisha, nyimbo hizi huwasilisha ujumbe fulani. Wadigo na Waswahili ni jamii mbili tofauti zenye asili na utamaduni tofauti mbali na mwingiliano wa kidini, kindoa na ujirani. Tatizo ni, je ujumbe unaowasilishwa na nyimbo za harusi katika jamii hizi mbili unafanana au ni tofauti. Mbali na kuwasilisha ujumbe, nyimbo pia hutekeleza majukumu fulani katika jamii kama vile, kuelimisha jamii kuhusu jambo fulani na kadhalika.

Je majukumu yanayotekelezwa na nyimbo za harusi za Wadigo yanafanana na yale yanayotekelezwa na nyimbo za harusi za Waswahili au la. Ujumbe unaowasilishwa na nyimbo za harusi huwa unalenga hadhira maalum katika jamii. Je hadhira inayolegwa na ujumbe katika nyimbo za harusi za Wadigo ni ile ile inayolengwa na ujumbe katika nyimbo za harusi za Waswahili au ni tofauti. Kulingana na tatizo tuliloangazia tumejishughulisha na uchambuzi linganishi wa maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili ili kubaini ukweli.

## **1.2 Madhumuni Ya Utafiti**

1. Lengo kuu la utafiti huu ni uchambuzi wa maudhui na majukumu yanayotekelezwa na nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili.
2. Katika utafiti huu tunalenga kulinganisha maudhui na majukumu katika nyimbo za harusi katika jamii hizi mbili, Wadigo na Waswahili.
3. Katika utafiti huu pia, tunalenga kubainisha walengwa wa ujumbe unaowasilishwa na nyimbo hizi za harusi.

### **1.3 Nadharia Tete**

Utafiti huu umejikita katika nadharia tete zifuatazo:-

- a) Kuna uhusiano mkuu kimaudhui kati ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili
- b) Kuna uhusiano wa karibu wa majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na zile za Waswahili.
- c) Hadhira inayokusudiwa katika nyimbo za harusi za Wadigo haitofautiani na ile ya nyimbo za harusi za Waswahili.

### **1.4 Sababu Za Kuchagua Mada**

Kilichonifanya nichague mada hii ni haja ya kutaka kujua katika nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili ni masuala gani yanayoangaziwa. Kuna haja ya kubainisha umuhimu wa nyimbo hizi katika sherehe za harusi. Pia kuna haja ya kubaini majukumu yanayotekelezwa na nyimbo hizi katika jamii husika. Haja ya kutaka kubainisha tofauti na usawa wa kimaudhui na kimajukumu unaodhihirika katika nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili.

Baada ya kupitia kazi mbalimbai zilizoandikwa kuhusu mada, niliona kuna pengo katika utanzu huu wa nyimbo kwamba baadhi ya nyimbo katika jamii zingine kama vile Wadigo hazijashughulikiwa kwa undani. Kile kimeshughulikiwa ni utaratibu wa harusi za Wadigo na za Waswahili kwa jumla. Uchambuzi linganishi wa nyimbo za harusi katika jamii hizi mbili haujafanywa. Hali hii imenifanya nichague mada hii, ili nizibe pengo lililopo katika uchambuzi wa nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Sababu nyingine iliyonifanya nichague mada hii ni kutaka kuchangia kimawazo katika fasihi simulizi. Nyimbo ni kipera kimojawapo kati ya vipera vya fasihi simulizi. Nyimbo zimezungumziwa kwa jumla kama vile aina za nyimbo, majukumu yake na kadhalika. Lakini kila jamii iko na nyimbo zake zenye kutekeleza majukumu

mbalimbali kuna haja ya kufanyia utafiti wa nyimbo za kila jamii. Hali hii itawaelimisha watu kutoka jamii nyingine kufahamu utamaduni wa jamii zingine. Hali hii ndivyo iliyonifanya nichague mada hii.

## **1.5 Upeo Na Mipaka**

Katika utafiti huu wa nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili tumejikita katika jamii ya Wadigo wanaoishi kusini mwa Mombasa, yaani Kwale na Waswahili wa Lamu. Wadigo wanapatikana katika sehemu mbalimbali za pwani. Sehemu hizi ni kama vile Likoni, Changamwe, Kisauni na Jomvu. Sehemu hizi zapatikana katika kaunti ya Mombasa. Katika kaunti ya Kwale, Wadigo wanapatikana Matuga, Mkongani, Tiwi, Msambweni, Kinondo, Lungalunga na kadhalika. Kwa kuwa jamii hii inaishi katika sehemu tofauti tofauti za pwani, itakuwa kazi ngumu kufanya utafiti katika sehemu zote wanapoishi. Kwa sababu hii, utafiti huu umejikita katika nyimbo za harusi za jamii ya Wadigo wa Tiwi pekee. Kama majirani wao Wadigo, Waswahili wanapatikana katika sehemu mbalimbali za pwani kuna wanaoishi Lamu, Jomvu, Mvita, Pate, Vanga, Funzi, Shimoni na kadhalika. Kwa sababu ya upana wa sehemu wanayoishi Waswahili, itakuwa vigumu kutembea sehemu hizo zote kukusanya data ya utafiti. Hivyo, katika utafiti huu tumejikita katika nyimbo za harusi za Waswahili wa Lamu pekee.

Kwa sababu ya umbali wa kimaeneo, jamii moja inayoishi sehemu mbalimbali hudhihirisha tofauti kama vile za kimatamshi na hata za shughuli za kitamaduni kama vile taratibu za ndoa na kadhalika. Kwa sababu hii, mbali na sehemu hizi mbili zilizoteuliwa kwa minajili ya utafiti, iwapo kutakuwa na habari ambazo ni muhimu katika utafiti huu na zinapatikana nje ya Tiwi na Lamu basi tutaangazia kwa minajili ya kufanikisha utafiti huu.

Nyimbo za harusi ni nyingi na zinaweza kuainishwa katika makundi mbalimbali. Kunazo zinazoimbwa na makundi ya kiasili hasa wanawake na kuna zile zinazoimbwa na bendi za kimuziki hasa taarab. Katika utafiti huu tumeshughulikia zile za makundi ya kiasili na pia zile za bendi. Idadi ya nyimbo za kiasili zilizoshughulikiwa katika jamii ya Wadigo ni sita na katika jamii ya Waswahili ni sita. Zile za bendi zilizoshughulikiwa ni mbili.

### **1.6 Msingi Wa Kinadharia Wa Utafiti**

Tumetumia nadharia ya uhalisia katika utafiti huu. Nyimbo ni utanzu katika fasihi simulizi. Kwa kuwa fasihi simulizi kama fasihi andishi inahusu binadamu na mazingira yake, kigezo tutakachotumia kupimia kazi hii ni msingi wa nadharia ya uhalisia. Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007). Dhana ya uhalisia ilianza kutumika takribani mnamo mwaka wa 1790. Katika mwaka huo, Emmanuel Kant katika chapisho lake lililoitwa '*Critique of Judgement*' aliitumia istilahi ya udhahania kamilifu kama kinyume cha uhalisia. Kufikia mwaka wa 1798, wahakiki kama vile Schiller walikuwa wakitumia maneno haya yaani udhanifu na uhalisia kuashiria vinyume.

Dhana ya uhalisia imekuja kuhusishwa na miktadha miwili. Kwanza inatumiwa kama njia ya kutathmini hali au halia. Huu ni uhalisia wa maisha. Uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Uhalisia unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Katika kitabu chake kinachoitwa *Aesthetics*, Hegel alilitumia neno uhalisia kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka.

Waandishi na wahakiki wengi waliotumia nadharia ya uhalisia, waliamini ya kwamba dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo. Mhakiki naye alimtathmini mwandishi



kwa namna ambayo huyo mwandishi alijibidisha kuonyesha ukweli. Haja kubwa ya kuigiza ilikuwa kuonyesha picha ya mazingira ambamo jamii inapatikana. Mwandishi anapaswa kutoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku. Tukirudi katika mada, nyimbo hasa za harusi huangazia mambo yanayodhihirika katika jamii. Mara nyingi nyimbo hutekeleza majukumu kama vile kukashifu, kukejeli na kusifu matendo yanayotendwa na wanajamii. Hii ndiyo sababu iliyopelekea kuchagua nadharia ya uhalisia.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) kazi ambazo zinaangaliwa kama za kihalisia, zinatarajiwa kuwa kama akisiko la hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika. Nadharia hii iliwekewa msingi na mwanafalsafa anayejulikana kama Hegel katika kitabu chake kinachojulikana kama Aesthetics. Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno hili kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inauwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kwa jinsi inayochochewa waziwazi na hali aliyomo.

Msingi mkubwa wa nadharia hii ni usimulizi wa kimuhakati. Huu ni usimulizi ambao unasimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inayokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii. Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya kijamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishi wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii.

Mawazo yanayodhihirika katika nyimbo za harusi huangazia hali au mambo halisi katika jamii. Kunazo zinazokashifu matendo ya wanawake dhidi ya mabwana zao ambayo yanaenda kinyume na maadili ya jamii husika. Wakati wa harusi nyimbo za aina hii huimbwa ili kumtahadharisha bibi arusi dhidi ya matendo hayo. Pia kunazo zinazosifu baadhi ya matendo ya wanaume dhidi ya wakezao. Huimbwa ili humuadilisha bwana arusi.

## **1.7 Yalioandikwa Kuhusu Mada**

Kunao wengi walioshughulikia utanzu wa nyimbo, Kuna wale walioshughulikia nyimbo kwa jumla na wale walioshughulikia nyimbo za jamii maalum. Mogambi (2007), ameshughulikia nyimbo kwa jumla. Ameangalia dhima ya nyimbo, maudhui ya nyimbo, sifa za nyimbo, umuhimu wa nyimbo na aina mbalimbali za nyimbo. Mbali na kwamba utafiti wetu ni kuhusu kipera cha nyimbo za harusi katika jamii mahususi, kazi hii imetusaidia katika uchambuzi wa maudhui.

Kirubi, Ngonje na Wandeo (2007), wameshughulikia nyimbo kwa jumla. Wameangalia dhana ya nyimbo, sifa za nyimbo, muundo wa nyimbo, aina za nyimbo na majukumu ya aina tofauti tofauti za nyimbo. Kazi hii imetufaa katika kushughulikia majukumu ya nyimbo za harusi. Beja (2000), alijishughulisha na utafiti wa nyimbo za matanga katika jamii ya Wagiriama. Aliangalia maudhui yanayodhihirika katika nyimbo hizi. Kazi hii imetusaidia jinsi ya kuchambua maudhui yanayojitokeza katika nyimbo. Timammy (2002), amefanyia utafiti nyimbo za harusi za jamii ya Waswahili. Katika utafiti wake alijikita katika nyimbo za harusi za wanawake Waswahili wa Mombasa. Ametafiti kuhusu mtindo wa nyimbo hizi za harusi. Kazi hii imetusaidia katika kuchambua nyimbo za harusi za Waswahili.

Mjomba (2011), alifanyia utafiti nyimbo za harusi katika jamii ya Wadawida. Utafiti wake umejikita katika nadharia ya upole, ambayo inatekeleza jukumu la kuokoa nyuso za maarusi kutokana na matusi yanayoangaziwa katika nyimbo hizi. Kazi hii imetusaidia jinsi ya kutambua maudhui katika nyimbo za harusi kwamba wakati mwingine ujumbe huwa umefichika.

## 1.8 Mbinu Za Utafiti

Mojawapo ya mbinu zilizotumika katika utafiti huu ni ya maktaba. Katika maktaba nimeurusu vitabu ambavyo vina habari muhimu kuhusu mada ya utafiti. Mbali na vitabu, katika maktaba nimesoma tasnifu za wataalamu walioshughulikia mada zenye ulinganifu na mada ninayoshughulikia. Mbinu nyingine iliyotumika katika utafiti huu ni kuwajiji baadhi ya wanajamii katika jamii husika wenye uelewa wa utaratibu wa harusi. Nimetumia hojaji ishirini na nne, mbili za utaratibu wa harusi na ndoa katika jamii ya Wadigo, mbili za utaratibu wa harusi na ndoa katika jamii ya Waswahili, kumi za maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na kumi za maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za Waswahili.

Katika mahojiano, nimewajiji watu ishirini na wanne. Watu hawa wamekuwa mchanganyiko wa wanawake na wanaume, umri wa wajijiwa ni kuanzia miaka thalathini na zaidi. Hii ni kwa sababu wamepevuka kiakili na wameshuhudia utaratibu na sherehe za ndoa mara kadhaa, kwa hivyo wanaufahamu wa mambo haya. Utafiti huu umefanywa Lamu na Tiwi.

Lamu imeteuliwa kwa kuwa Waswahili wanaoishi sehemu hiyo bado wanahifadhi utamaduni wao kwa kuwa hawajaingiliana sana na watu kutoka jamii nyingine tofauti.

Wadigo wa Tiwi bado wanaendeleza utamaduni wao licha ya kwamba wameingiliana na watu wengine kutoka bara na nchi zingine. Hii ndio sababu iliyonifanya nichague sehemu hizi katika utafiti huu. Mbinu nyingine muhimu sana ni kwenda nyanjani. Nimehudhuria sherehe za harusi nyanjani ili kupata kujua namna sherehe za harusi zinavyoendeshwa, pia kusikia nyimbo zinazoimbwa katika sherehe hizo. Ushauri kutoka kwa wahadhiri hasa wasimamizi katika utafiti huu umechangia katika ufanisi wa shughuli nzima ya utafiti.

## **1.9 Hitimisho**

Katika sura hii tulianza kwa kueleza kuhusu jamii ya Wadigo na Waswahili, jinsi walivyolingiliana katika shughuli zao za kila siku. Pia tumeangazia athari za mtagusano wao. Isitoshe tulieleza tatizo la utafiti na madhumuni kwa kujikita katika nadharia tete tulizoziteua. Pia tumeelezea sababu za kuchagua mada, kisha tukaeleza kuhusu upeo na mipaka ya utafiti. Tumezungumzia kuhusu msingi wa nadharia ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.

## **SURA YA PILI**

### **HARUSI NA NDOA**

#### **2.0 UTANGULIZI**

Katika sura hii tutajikita katika utaratibu wa harusi na ndoa katika jamii ya Wadigo na Waswahili. Katika jamii hizi mbili shughuli ya harusi na ndoa ni shughuli muhimu sana katika maisha. Hii ni kwa sababu kupitia sherehe hii mtu hutoka katika ujana na kuingia katika utu uzima. Kama tulivyoangazia katika sura ya kwanza kwamba watu kutoka jamii hizi mbili ni wafuasi wa dini ya kiislam. Katika Korani tukufu na hadith za mtume, jambo la ndoa limetiliwa mkazo.

Inasemekana ni njia moja ya kupata utulivu kwamba mtu akioa au akiolewa hupata utulivu. Pia yasemekana ukitekeleza jambo hili la ndoa, ni sawa na kutekeleza nusu ya dini ya kiislamu. Wanaoowana huwa wametekeleza nusu ya imani yao na ile nusu iliyosaliya ni swala, saumu, zakati, kuenda kuhiji na amali zengine. Hii ndiyo sababu shughuli hii hutiliwa manani sana katika jamii hizi mbili.

#### **2.1 Utaratibu Wa Harusi Na Ndoa Za Wadigo Wa Tiwi**

Katika jamii ya Wadigo, shughuli ya harusi na ndoa hufuata utaratibu maalumu tokea mwanzo wawili wanapopendana hadi nikaha inapofungwa na sherehe zote kuisha. Utaratibu nitakaoelezea niliupata baada ya kuwahoji wanaume na wanawake kadhaa katika jamii husika. Hassan Suleiman Kuchengwa na bibi Halima Rama Sudi kutoka Tiwi ni baadhi ya wale waliohojiwa.

### **2.1.1 Posa**

Posa ina maana ya kupeleka maombi ya kutaka kuoa kwa wazazi wa binti anayetarajiwa kuolewa. Pia posa ina maana ya maombi ya kutaka kuowa yanayopelekwa kwa wazazi wa binti anayetarajiwa kuolewa. Katika jamii ya Wadigo, mvulana na msichana katika matembezi yao ya kila siku, hukutana wakapendana na wakakubaliana waowane. Jambo hili huchukua muda. Muda unaochukuliwa na wachumba kabla ya kuowana hutegemea na nafasi ya mvulana. Kunao wanaochukua mwezi moja wengine huchukua hata mwaka.

Mvulana anapopata mchumba na kuwa tayari kumuoa, huwakalisha wazazi wake yaani baba na mama na kuwaeleza kuhusu nia yake ya kutaka kuoa, na pia msichana anayemkusudia kumuoa. Baada ya wazazi kuelezewa nia ya mvulana wao na msichana anayetarajia kumuoa, huanza kufanya uchunguzi kumuhusu msichana huyo. Uchunguzi huu huhusisha mambo kama vile tabia na mienendo yake, asili na fasili ya familia yake na kadhalika. Habari hizi hupatikana kupitia majirani wa karibu wa familia ya msichana.

Wanaporidhika na habari kuhusu msichana anayetarajiwa kuolewa na mtoto wao, kwamba ana tabia nzuri na asili ya familia yao ni nzuri yaani haina historia ya visa vyovyote vibaya, hupanga kutuma watu watakaoenda kwa wazazi wa msichana kupeleka posa. Kabla ya kwenda kupeleka posa, hupeleka habari kuhusu siku wanayotarajia kwenda kukutana na familia ya msichana. Familia ya msichana inapopata ujumbe wa siku ya kuwasili kwa wageni, hujiandaa. Kwanza huitisha mkutano wa familia. Kikao hiki huhusisha ndugu wa babake msichana. Wanaume na wanawake huhudhuria kikao hiki. Mambo yanayojadiliwa huwa ni mahitaji ambayo watapewa wale watakaoleta posa.

Mahitaji haya huwa ni ada ambayo ni itolewe ndipo wapewe idhini ya kuoa. Ada hii huhusisha pesa na vyakula. Mahitaji hayo huorodheshwa kwenye karatasi na baadaye huwekwa kwenye bahasha, ambayo itakabidhiwa wale watakaoleta posa. Katika orodha huwa:

### **Kilemba na maziwa.**

Huwa ni pesa ambazo hupewa wazazi wa msichana. Hakuna kiwango maalumu, hutegemea matakwa ya familia. Kunazo familia ambazo hutaka shilingi laki moja na wengine hutaka shilingi elfu thamanini au sitini. Pesa hizi zinapotolewa hugawanywa mara mbili. Migao hii huitwa kilemba na maziwa. Kilemba hupewa baba na maziwa huwa ni ya mama. Kwa kuwa mtoto katika jamii huwa si wa mtu mmoja bali huwa ni wa familia, pesa za kilemba ambazo ni za baba hugawa ndungu zake wanaume kwa wanawake. Huwagawia kiasi tu lakini yeye mwenyewe hubaki na kiasi kikubwa. Mama naye hugawa zile pesa za maziwa na ndugu zake, wanaume kwa wanawake.

### **Mahari**

Mahari ni zawadi anayopewa msichana na mvulana anayemwoa. Zawadi hii huhusisha vitu tofauti tofauti kama vile mapambo ya nyumba yaani fanicha, pesa, msahafu, vitu vya dhahabu kama vile mkufu, vipuli, pete na kadhalika. Familia itaamua msichana wao apate mahari ya aina gani.

### **Chidzufyu (Pesa za mashemegi)**

Hii ni ada ya kiasi fulani cha fedha ambazo hupewa ndugu wa msichana yaani mashemegi. Pesa hizi lengo lake ni kuwajulisha kuwa dada yao anaolewa. Hakuna kiwango maalumu cha pesa hizi. Kunao wanaoitisha elfu tatu na wengine huitisha hata elfu nne.

## **Mchele**

Jamaa wa mvulana anayetaka kuoza, huagizwa mchele kiasi kinachohitajika huwa mara nyingi ni kilo mia moja. Mchele huo huwa ni zawadi kwa familia ya msichana. Kwa kuwa mtoto katika familia ni wa kila mtu, mchele ule huwekwa hadi siku ya harusi. Hupikwa na kuliwa na kila aliyehudhuria harusi.

## **Mbuzi**

Mbuzi wanaohitajika katika orodha ya mahitaji huwa wawili. Mbuzi hawa, kama vile mchele huwa ni zawadi kwa familia ya msichana. Huchinjwa wakati wa sherehe ya harusi kama kitoweo cha wali utakaopikwa.

## **Kamba**

Mbuzi watakaopelekwa huhitaji kamba za kuwafunga. Kamba hizi huwa si kamba za kawaida kama vile za manila bali huwa lesu. Mbuzi wenyewe huwa wawili na lesu nazo huwa gora mbili. Lesu zinazohitajika huwa ni zile ngumu yaani mali ya Abdhallah.

## **Blanketi**

Blanketi hili huwa ni zawadi ya wazazi wa msichana. Zawadi hii hujumuisha vitu kama vile saruni ambayo huwa ni ya babake msichana na shiti moja ambayo huwa ni ya mamake msichana. Mafuta ya uto mtungi mmoja wa lita ishirini. Ngano bandali moja yaani kilo ishirini na nne. Unga wa sima bandari moja yaani kilo ishirini na nne. Sukari kama kilo ishirini na tano. Vitunguu maji neti moja, dawa za pilau, vitunguu saumu neti moja maziwa ya unga kama kilo kumi. Tomato kreti moja viazi kreti moja, majani, hamira, tomato mkebe, iliki.

Baada ya kuorodhesha vyombo ambavyo familia ya mvulana wanahitajika kupeleka kwa familia ya msichana, mashangazi hufanya kikao chao kutayarisha orodha nyingine ya vyombo. Orodha hii huitwa kikapu cha uchumba. Vyombo hivi hugawika mara mbili. Mgao wa kwanza



huwa mavazi na bidhaa zingine za kufanyia usafi. Vyombo hivi huwa ni zawadi ya msichana anayechumbiwa kutoka kwa mvulana yaani mchumba wake. Mgao wa pili huwa vyakula, navyo huwa zawadi kwa mamake msichana anayeolewa. Vyakula hivi vinapoletwa, mamake msichana hugawa na kungwi ambaye atamweka msichana ndani na kumfunza mambo yanayotakikana kwa mwanamke.

Baada ya mashangazi kuorodhesha vyombo vinavyohitajika katika kikapu cha uchumba, huweka orodha hiyo kwenye bahasha.

Siku ya kupeleka posa inapowadia, wanaume wawili na wanawake wawili kutoka kwa familia ya mvulana huenda kupeleka posa. Wanaume hawa wanaweza kuwa ni babake na ami yake mvulana nao wanawake huwa mashangazi wa mvulana. Wakifika nyumbani kwa familia ya msichana, huwa kuna watu wa familia hiyo ambao wanawasubiri. Baada ya salamu, hutakikana wajitambulisha kuwa wanatoka wapi na wameenda pale kwa lengo gani. Harakati hii huitwa “kubisha hodi”. Kabla ya kujitambulisha huwa kuna ada ambayo ni watowe ada yenyewe huwa ni kiasi fulani cha fedha. Hakuna kiwango maalumu, huanzia shilingi mia tatu hadi elfu moja. Baada ya kutoa ada ya kujitambulisha, wenyeji watawaitikia “yoo”.

Watajieleza kwamba wao ni akina nani na lengo lao la kufika hapo ni nini. Wenyeji wao watawambia ya kwamba hawajasikia. Kuna ada ambayo ni watoe inayoitwa kifungua masikio. Ada hii huwa ni pesa ambazo huitishwa na familia ya msichana. Pesa hizi hazina kiwango maalumu. Wanaweza kuitisha shilingi elfu tatu. Kwa kuwa hakuna kiwango maalumu, si lazima watoe kile wameitishwa lakini wanaweza kutoa kiasi kinachokaribiana na kile wameitishwa. Kwa mfano, wanaweza kutoa shilingi elfu mbili au elfu mbili na mia tano.

Wakishatoa ada hiyo, wataambiwa kuwa wamewafungua macho na masikio.

Wataambiwa waseme kilichowapeleka. Watasema kuwa wameenda kuposa. Wataambiwa watoe ada ambayo huwa ni pesa lakini hakuna kiwango maalumu. Ada hii inaitwa ‘buru la mhalani’. Wakishatoa ada hii watakabidhiwa zile bahasha mbili za mahitaji yanayotakikana kabla ya kupewa ruhusa ya kuoa.

### **2.1.2 Kupeleka mizigo**

Mizigo ina maana ya yale mahitaji au vile vyombo na pesa zilizohitajika katika familia ya msichana baada ya kupeleka posa na kukabidhiwa zile bahasha mbili zenye mahitaji yaliyoitishwa na familia ya msichana, familia ya mvulana huitisha mkutano wa ndugu kuja kujadili jinsi watakavyo fanya ili kutimiza vyombo vilivyotakikana. Katika mkao huo huangaliwa gharama yote ya shughuli nzima. Kila mtu katika familia hupewa jukumu la kutekeleza. Kunao watakao pewa kiwango fulani cha pesa ili kuchangia kilemba na maziwa. Kijana anayeowa huhitajika kutoa kiwango kikubwa cha pesa zilizohitajika. Kwa mfano kama kilemba na maziwa ni elfu sitini huhitajika kutoa elfu thalathini na zile zilizobaki huchangiwa na familia.

Mahari ambayo ni zawadi ya msichana kutoka kwa mvulana hutolewa na mvulana bila usaidizi wa mtu yeyote. Pesa zitakazochangwa, mbali na kugharamia kilemba na maziwa zingine zinatajikana kununua vyombo kama vile mchele, ngano, uto, samli na kadhalika. Hivi ni vile vyombo vinavyohitaji pesa nyingi ambazo haziwezi kutolewa na mtu mmoja. Vyombo vingine vyenye gharama ndogo hukabidhiwa watu wavinunue na baadaye wapeleke nyumbani kwa akina mvulana. Vyombo vya kikapu cha uchumba hugawanywa wanawake, kila mmoja atanunua kile amepewa na kupeleka nyumbani kwa akina mvulana.

Baada ya mchango na kuhakikisha kwamba vitu vyote vilivyoitishwa vimetimia na pesa zilizohitajika zimepatikana, kikao huitishwa ili kujadili kuhusu siku muafaka ya kupeleka mizigo hiyo kwa familia ya msichana. Wanapokubaliana siku watakayo peleka mizigo, huarifu familia ya msichana ili wajiandae kusubiri wageni.

Siku ya kupeleka mizigo ifikapo, watu kadhaa wake kwa waume kutoka familia ya mvulana hukutana nyumbani kwa wazazi wa mvulana kukagua mizigo kama imekamilika na pia kujiandaa kupeleka mizigo hiyo. Kwa sababu mizigo huwa ni mingi na watu pia huwa wengi kiasi, gari hukodishwa kupeleka msafara huo. Shughuli hii huanza asubuhi sana nyumbani kwa akina mvulana.

Kabla ya safari kuanza, huwa na kiamsha kinywa ambapo wanawake hutayarisha mahamri na chai. Baada ya kiamsha kinywa mizigo hutolewa nje na kufungwa mafurushi kwa kutumia lesa, mbuzi nao hufungwa kamba za lesa, vyombo vya kikapu cha uchumba huwekwa kwenye kikapu na baadaye kufungwa furushi la lesa. Baadaye mizigo hiyo huingizwa kwenye gari na wenyewe pia huabiri gari tayari kuelekea nyumbani kwa wazazi wa msichana.

Kwa upande wa familia ya msichana wakiletewa habari ya siku ya kuletwa kwa mizigo, hualika ndugu kuja kupokea wageni na mizigo. Siku hiyo ya kuletwa kwa mizigo, huwa na maandalizi ya chakula cha wageni, mara nyingi wageni hawa hutayarishiwa rojo la viazi mahamri, chapati na chai.

Wakati wa kupeleka mizigo wanaopeleka, hasa wanawake, huimba nyimbo wakati wanapoelekea kwa kina msichana. Wanapotoka nyumbani kwa akina mvulana huimba wimbo kama vile,

*Salama we navoya Salama*

*Salama*

*Kulola kure nikumanya siri za atuu*

*Siri za atu zinahadza kaya hino*  
*Chivyere anamba*  
*Samahani we navoya*  
*Salama salama*

**Tasfiri**

Salama naomba Salama  
Kuowa mbali ni kujua siri za watu  
Siri za watu zataja mji huu  
Babake bibi harusi anasema;  
Asamehewe, anaomba Salama

Wimbo huu huimbwa mpaka wanapokaribia kwa akina msichana hubadili wimbo mwingine wa kuingilia kwenye boma la wazazi wa msichana. Wimbo wenyewe ndio huu:

*Hino nyumba ya myao*  
*Mpaka ubishe hodi*  
*Chivyere nakula Musa*  
*Hodi hodi chivyere nakulamusa*  
*Uphapha wehebu ukauka*  
*kare nikedza.*

**Tafsiri**

Nyumba ya mwenzio  
Mpaka ubishe hodi  
Chivyere nakusalimia  
Hodi hodi Chivyere  
Nakusalimia  
Uko au umeondoka  
Nishakuja.

Wakishuka kutoka kwenye gari na washukishe mizigo hiyo huimba na kucheza ambapo huitwa kung'ara. Wimbo unaoimbwa ni kama vile:

*Mduruma na Mdigo*

*Reroandangwirana*

*Reroandangwirana mayowe*

*Naphiha Golini nikalole mwanagwa*

*Mwanagwa wahenda vyalika*

*Chivyere we unaphayaphaya*

*Mduruma na Mdigo*

*Reroandangwirana*

### **Tafsiri**

Mduruma na Mdigo

Leo Watashikana

Naenda Golini

Nikaowe mtoto wa wenyewe

Mtoto anapendeza

Chivyere unamchezo

Jamii mbili tofauti

Leo zitashirikiana.

Wanawake kutoka familia ya msichana na hasa mashangazi watachukua shiti kubwa na kuenda kupokea kikapu cha uchumba kutoka kwa wanawake waliokuja. Mzigo huo utafinikwa shiti pamoja na wenyewe na waelekee nyumbani ambako utaenda kukaguliwa iwapo vitu walivyoagiza vimeletwa vyote. Wakifika chumbani ambamo kikapu kitafunguliwa, huwa kuna kungwi ambaye ndiye atakayemweka mwari. Kungwi ataimba kuomba ufunguo wa kufungulia mzigo.

*Navoya Mshomoro*

*Niombole ndembo*

*Yangu wee*

**Tafsiri**

Naomba ufunguo

Nifungue mzigo

Wangu

Mwanamke mmoja kati ya wale wageni ambaye amepewa pesa za ada ya kufungulia mzigo huitikia.

*Nakupha Mshomoro*

*Uombole ndembo wee*

**Tafsiri**

Nakupa ufunguo

Ufungue mzigo wako

Anapopokea pesa hizo ambazo hazina kiwango maalum huagiza mzigo ufunguliwe ile lesu. Vyombo hukaguliwa kimoja baada ya kingine mpaka viishe kwenye kikapu huku wakiangalia na orodha waliyoandika kuhakikisha kuwa vyote vimeletwa. Kwa kuwa huwa ni vyombo visivyo na gharama kubwa, huwa vinanunuliwa vyote.

Wakati wanawake wakishughulika na vyombo katika kikapu cha uchumba, wanaume nao hushughulika na ile mizigo mingine. Babake msichana na ndugu zake hukagua mizigo hiyo kulingana na orodha ya vitu walivyoitisha. Kwa kuwa mahitaji haya yana gharama kubwa mara nyingi hayatimizwi yote. Kwa mfano pesa za kilemba na maziwa huwa si rahisi kutolewa kwa wakati mmoja. Mahari pia wakati mwingi huanzwa tu na kiasi kinachosalia hutolewa wakati mwingine. Vitu vile vingine kama mchele, ngano, mbuzi na vinginevyo huwa vyapelekwa vyote.

Baada ya mizigo kukubaliwa familia ya mvulana huomba idhini ya kutaka kuoambapo familia ya msichana hukubali ombi hilo. Tarehe ya harusi hupangwa siku hiyo na pande zote

mbili hukubaliana siku maalumu ya kufanyika kwa sherehe hiyo. Mazungumzo yanapofika kikomo, wageni huandaliwa chakula. Wakishamaliza kula, huingia kwenye gari iliyowaleta tayari kurudi nyumbani. Wakati wa kupeleka mizigo, wanawake kutoka familia ya mvulana hukabidhiwa barua yenye mahitaji yanayoitwa begi ambayo hutayarishwa na mashagazi na kungwi wa msichana.

### **2.1.3 Matayarisho ya harusi**

Matayarisho haya yanahusu gharama ya shughuli nzima ya harusi. Familia ya mvulana huitisha mkutano wa ndugu kuja kujadili jinsi watakavyo simamia sherehe ya harusi. Mkutano huu hufanyika punde tu baada ya kupeleka mizigo na kupewa tarehe ya kufanyika kwa harusi. Kikao hiki ujumuisha ndugu wa babake mvulana na ndugu wa mamake mvulana.

Matayarisho haya hujumuisha vyakula vitakavyoliwa katika sherehe na pia tafrija mbalimbali zitakazotumika katika sherehe. Vyakula ambavyo huliwa katika sherehe hii huwa ni biriani, pilau, wali mweupe, chapati, mahamri, chai nakadhalika. Jukumu la kununua vyakula hivi huwa ni la pande mbili, ndugu wa baba na wa mama. Watu wa kwa baba hutakikana wanunue mchele, ngano, dawa za pilau, sukari, majani na hamira, maziwa, unga wa sima vyombo hivi huwa havitolewi pesa bali kila ndugu hukabidhiwa kile ataleta.

Kwa mfano ikiwa sherehe itahitaji kilo mia moja za mchele, basi huenda ukakabidhiwa watu watano ili kila mmoja anunue kilo ishirini. Ndugu wa mama hutakikana kugharamia mboga. Mboga hizi huwa ni nyama mbali na nyama pia hutakikana wanunue tomato, viazi, samli, uto, vitunguu. Kama vile wale ndugu wa baba kila mtu hukabidhiwa kile ataleta. Mbali na mankuli, kuna vyombo vya begi ambavyo huhitajika kununuliwa. Vyombo hivi hukabidhiwa wanawake. Mashagazi, mama wadogo, mashemegi na madada wa bwana harusi ndio hukabidhiwa kila mmoja chombo cha kununua.

Wakati familia ya mvulana ikifanya matayarisho ya harusi, pia familia ya msichana hufanya maandalizi ya sherehe ya harusi. Kwa kuwa huwa wamepokea mizigo na kuhifadhiwa hadi siku ya harusi kugharamia mahitaji ya sherehe, familia ya msichana huchangisha pesa kugharamia mahitaji madogo madogo kama vile nguo ya nikaha ya msichana, ngoma ya mchana ya usiku na pia kuongezea chakula iwapo kilicholetwa hakitoshi.

Wanaohusishwa katika kuchanga ni pande mbili, ndugu wa baba na mama wa msichana anayefanyiwa harusi.

#### **2.1.4 Harusi**

Sherehe ya harusi hufanyika pande zote mbili yaani kwa familia ya msichana na ya mvulana. Siku moja kabla ya harusi, familia zote mbili hudondoa. Hii ni siku ambayo mchele hutayarishwa kwa kutolewa taka na kupepetwa. Mbali na kudondoa, mahamri pia hutayarishwa wakati huu lakini hutengenezwa jioni baada ya kudondoa. Shughuli ya kudondoa huanza saa nane mchana.

Majirani wanawake hujumuika katika familia yenye harusi kwa shughuli hiyo ya kudondoa. Waliohudhuria hutayarisha visheti na chai rangi kama chakula chao. Shughuli hii huandamana na nyimbo.

Katika familia ya msichana, wakati wanawake wakiwa wanadondoa bibi arusi huwa anapambwa. Kwa kuwa huwa amewekwa ndani na kungwi na haruhusiwi kutoka nje, shughuli ya kupambwa hufanyika pale nyumbani au wakati mwingine gari huletwa hadi mlangoni akaingia na kupelekwa kwa mpambaji bila kuonekana na watu.

Mapambo huhusisha kupaka hina, kuchora piko na kuweka dawa nywele na kusetiwa.



Mnamo saa mbili usiku, upishi wa chakula cha sherehe huanza. Mara nyingi huwa ni pilau na angalabu sufuria moja ya wali mweupe. Kwa akina msichana huwa na sherehe usiku wa kuamkia siku ya nikaha. Sherehe hii huandamana na muziki wa taarab. Ngoma huanza saa nne usiku. Nje ya nyumba ya wazazi wa msichana huwekwa chandarua. Mara nyingi huwa kuna cha wapigaji ngoma na cha wachezaji. Ifikapo saa sita usiku bibi arusi hutolewa nje na kungwi wake hadi kwenye chandarua. Wimbo spesheli wa kumkaribisha hupigishwa.

Anapoingia kwenye chandarua, hucheza kwa mda kidogo na baadaye hukaa kwenye kochi ambalo huwa ameekeka. Muziki husitishwa na mfawiji wa sherehe hushika hatamu. Sherehe hii hujulikana kwa jina 'party'. Bibi arusi hutuzwa kwa kupewa pesa. Huwa na utaratibu maalumu wa kuendesha shughuli hii. Wazazi wa msichana ndio huanza kutoa pesa, ndugu wa msichana, wajomba na mashangazi. Familia wakiisha marafiki nao hutowa kile wangetaka kumzawadi bibi arusi. Shughuli ya kutuza inapoisha bibi arusi huregeshwa ndani, muziki hupigwa huku watu wakicheza. Hali hii huendelea hadi saa kumi alfajiri. Wenye muziki hufunganya virago vyao na kuenda. Matayarisho ya chakula kama vile rojo la viazi na chai hutayarishwa wakati huu. Pilau, wali mweupe na mahamri huwa yako tayari.

Katika familia ya mvulana huwa hakuna sherehe yoyote usiku wa kuamkia harusi. Jambo wanalofanya ni kuchagua wale watakuwa katika msafara wa kuenda kufuata bibi arusi wakiandamana na bwana arusi. Mara nyingi huwa marafiki wa bwana arusi, wajomba wawili au watatu, mashangazi na madada wa bwana arusi. Gari hukodishwa kuwapeleka kwa akina msichana.

Wakati mwingine huandamana na kadhi au kadhi hutoka kule kwa msichana. Msafara huanza safari mapema kwa maombi mnamo saa kumi alfajiri iwapo kwa msichana ni mbali. Hii

ni kwa sababu ndoa ikafungishwe asubuhi ili warudi waje wajiandae kwa sherehe ya usiku. Mashangazi wa mvulana ndio hubeba begi la bibi arusi.

Ifikapo saa kumi na mbili asubuhi, msafara wa bwana arusi huwasili nyumbani kwa akina bibi arusi. Mashangazi wa bibi arusi hupokea begi. Utaratibu wa kupokea begi ni kama ule wa kikapu cha uchumba. Begi hupokelewa na kupelekwa chumbani kwa bibi arusi. Kisha kungwi na mashangazi hukagua vyombo vilivyo ndani ya begi. Wakati wakiendelea kukagua begi, bwana arusi na wanaume wengine alioandamana nao huwa kwenye chandarua ambako kumewekwa mikeka tayari kwa nikaha. Kwenye chandarua mzazi wa kiume wa bibi arusi na jamaa zake pamoja na wengine walioalikwa huwa wameketi wakisubiri ndoa ifungishwe.

Wanawake huwa na chandarua chao ambapo hukaa na kusubiri ndoa ifungishwe. Baadhi ya wanawake ambao ni jamaa wa karibu wa bibi arusi huwa ndani kwa bibi arusi.

Kabla ya nikaha, kadhi na shahidi wa msichana huingia kwa bibi arusi kupata idhini yake ya kutaka kuolewa na bwana arusi. Ndani huwa na kungwi wake. Huulizwa mara tatu kama amekubali kuolewa na kijana anayetaka kumuoa. Baada ya kukubali, kadhi na shahidi hutoka na kuenda kwenye chandarua.

Bwana arusi naye huulizwa mara tatu kama amekubali kumuoa msichana anayetaka kuozwa. Anapokubali nikaha hufungishwa, huwa ni dua kutoka kwa Korani tukufu. Baada ya nikaha huwa na mawaidha yanayotolewa na kadhi au maalim yeyote aliyehudhuria sherehe hiyo. Mawaidha yanayotolewa huwa yanahusu maisha ya ndoa kwa jumla na umuhimu wa ndoa katika maisha ya mwanadamu. Shughuli za nikaha zinapofika kikomo, bwana arusi na msimamizi wake huenda kwa bibi arusi. Bwana arusi hupeana mkono kwa bibi arusi. Katika hali hii, bwana arusi hupeana kiasi fulani cha fedha kwa bibi arusi kama zawadi.

Baada ya kutoa mkono hupewa vyakula ambavyo huwa vimetayarisha kwa ajili yake. Vyakula hivi ni chai ya maziwa, tambi, keki, mkate wa sinia, mkate wa tambi na kadhalika. Bwana arusi hula vyakula hivi chumbani mwa bibi arusi pamoja na bibi arusi. Shughuli hii huenda sambamba na upigaji picha.

Baada ya chai na vitafunio huandaliwa wali kwa kuku wa kupika. Chakula hiki hujulikana kama kombe la bwana arusi. Wakati bwana arusi na msimamizi wake wakila kombe, nje waliohudhuria pamoja na msafara wa bwana arusi hupewa chakula. Chakula chenyewe huwa pilau au wali mweupe kwa wale wasiokula pilau, chai, mahamri, rojo la viazi. Shughuli ya kula inapoisha, huwa na muda kama jisaa jimoja la kupeana zawadi kwa bibi arusi. Zawadi hizi huwa vyombo vya nyumbani kama vile sahani, vikombe, sufuria na kadhalika. Zawadi hizi hutolewa na mashangazi, mama, mama wadogo, dada na marafiki wa bibi arusi.

Shughuli ya kumzawadi bibi arusi huenda sambamba na upigaji picha. Kufikia kiwango hiki, shughuli ya harusi huwa imeisha kwa jamii ya msichana. Vyombo vya bibi arusi hufungwa katika mizigo tofauti tofauti na kuwekwa kwenye gari iliyokuja na bwana arusi, tayari kuelekea kwake. Watu wanaoandamana na bibi arusi kuelekea kwa bwana arusi ni kungwi wake na dada zake kama wawili.

Msafara unapofika kwa bwana arusi, hukaribishwa kwa nyimbo na vigelegele. Bibi arusi huingizwa chumbani nyumbani mwa bwana arusi. Chumba huwa kimenadhifishwa kwa mashiti mapya, zulia, pazia kila kitu huwa ni kipya. Baada ya kukaribishwa hupelekewa chakula pamoja na wale walioandamana naye kutoka kwao kama vile kungwi. Wakati bibi arusi akila, jamaa na wageni waalikwa hupewa chakula. Chakula huwa pilau au biriani na wali mweupe kwa mchuzi. Wamalizapo kula, huanza matayarisho ya sherehe ya usiku. Bibi arusi hupelekwa kwa

mpambaji. Nywele hutengenezwa kwa namna tofauti mbali na vile zilivyotengenezwa wakati wa nikaha.

Chakula huwa kimebakishwa cha wale watakaohudhuria sherehe ya usiku, ifikapo jioni mnamo saa moja waliohudhuria hupewa chakula. Chandarua huwa kimewekwa kwa ajili ya ngoma ya usiku ambayo huwa ni taarab. Mnamo saa mbili usiku mziki wa taarab huanza. Wake kwa waume huingia kwenye chandarua kucheza kwa raha zao. Ifikapo saa nne usiku kuelekea saa tano, bwana arusi hupishwa uwanja kwenye chandarua. Huchagua wimbo aupendao apigiwe wakati wa kuingia. Hucheza kidogo na kukaa kwenye kochi akisubiri bibi arusi. Punde si punde bibi arusi hupigiwa wimbo aupendao wa kuingilia kwenye chandarua. Huingia kwa madaha huku akicheza, huwa ameandamana na viandama wake.

Afikapo kwenye chandarua huungana na bwana arusi na kucheza pamoja. Huachiwa uwanja kwa muda mpaka wimbo uliochaguliwa na bibi arusi ufike tamati ndipo wote wawili hukaa kwenye kochi. Mfawidhi wa sherehe huchukua hatamu na kuanzisha shughuli ya kuwatuza maarusi hao. Utaratibu wa sherehe hii huanza na wazazi wa bwana arusi kuwatuza maarusi hao, ndugu, jamaa na marafiki huwatuza maarusi hao. Zawadi zinazopeanwa ni pesa, nguo, vyombo vya nyumbani na kadhalika. Shughuli hii huandamana na upigaji picha. Shughuli hii huchukua muda wa masaa mawili. Mnamo saa sita usiku shughuli ya kuwatuza maarusi hufika tamati. Maarusi huenda nyumbani mwao kulala huku wakiacha waliohudhuria kuendelea kucheza. Ifikapo saa kumi asubuhi, mziki huachwa kucheza na wapigaji mziki huo hufunganya virago vyao tayari kuondoka. Waliohudhuria nao hufumukana kila mmoja huenda kwao, ishara kwamba sherehe imefikia tamati.

Baada ya harusi, bibi arusi hukaa ndani siku saba. Siku ya nane hutolewa nje na huwa huru kutangamana na jamaa katika familia ya bwana arusi.

## **2.2 Utaratibu Wa Harusi Na Ndoa Za Waswahili Wa Lamu**

Kama jamii ya Wadigo, Waswahili hufuata utaratibu maalumu katika shughuli zao za harusi na ndoa. Utaratibu huu ulitolewa na Thureya Ali Yusuf na Mariam Mjahidi kutoka Lamu.

### **2.2.1 Posa**

Mvulana anapokutana na msichana wakapendana na kuamua kuwana, huwaeleza wazazi wake yaani baba na mama. Baada ya wazazi wa mvulana kupewa habari na kijana wao kutaka kuo, hutafuta rafiki wa karibu wa babake msichana anayekusudiwa kuolewa na kijana wao. Rafiki wa babake msichana hupewa salamu za kutaka kuposa awapelekee wazazi wa msichana. Babake msichana akipata salamu za kupendwa kwa binti yake, humueleza mkewe salamu hizo. Mamake msichana huzungumza kuhusu jambo hilo na binti yake. Kwa kuwa msichana huwa tayari amekutana na mvulana na wakapendana, hukubali kuwa yutayari kuolewa na kijana anayetaka kuleta posa. Watu kutoka familia ya msichana kama vile wajomba, mashangazi na wengineo hukutana na kujadili kuhusu kiwango cha mahari wangependa kupewa msichana wao. Mara nyingi mahari huhusisha kiasi fulani cha fedha na fanicha. Kwa mfano wanaweza kukubaliana kiwango cha fedha kuwa elfu hamsini na fanicha.

Baada ya familia ya msichana kukutana na kujadili kiwango cha mahari, babake msichana hupeleka salamu kwa wazazi wa mvulana kuwa wanaweza kuenda kupeleka posa. Ujumbe unapowafikia wazazi wa kijana, hupeana siku ambayo wataenda kuposa. Wakati wa kupeleka posa, babake mvulana huandamana na mjomba wa mvulana na rafiki yake wa karibu. Wakifika kwa akina msichana huwa familia wanawasubiri. Mazungumzo huanza na katika harakati hiyo, jamaa wa msichana huwambia kiasi cha mahari ambayo yanahitajika yaani kiasi fulani cha fedha na fanicha. Iwapo kiasi cha mahari kilichotajwa kulingana na uwezo wao kiko

juu, basi wanahiyari ya kutaka kupunguziwa kwa kuwa kuoza na kuoza ni jambo la heri, familia ya msichana hawana budi kupunguza. Mbali na mahari pia huambiwa wapeleke begi.

Begi huwa ni vyombo ambavyo hupelekewa bibi harusi. Vyombo hivi ni kama vile lesa, shiti, viatu vya chooni na safari, mafuta ya kujipaka, tauli, chupi, vitambaa vya kanzu, robu, mswala, msahafu, buibui nakadalika. Baada ya kuelezwa mahitaji yanayotakikana, hurudi nyumbani kuenda kutayarisha ada waliyotakikana kutowa. Kabla ya kuondoka watu wa kina bwana wataomba mda wakatayarisha mahari waliyoambiwa watowe. Hakuna mda maalum, hutegemea uwezo wa familia ya bwana na kiasi cha mahari walichoambiwa. Kwa mfano huenda ikawa majuma matatu au mwezi.

Katika jamii ya Waswahili, mahari ni jukumu la kijana anayetaka kuoza kutayarisha kiasi cha mahari yaliyohitajika. Iwapo hana uwezo wa kutosha, jamaa zake wa karibu kama vile babake, kaka zake ndio huchanga kumsaidia gharama hiyo ya mahari. Baada ya posa, msichana huekwa ndani haruhusiwi kutembea mtaani kwa kuwa amekuwa mchumba wa kijana anayetarajiwa kumuoa. Akiwa ndani hushughulikiwa na mamake na mashangazi. Shughuli kubwa huwa ni kumpatia mafunzo kuhusu namna ya kuishi na bwana, jinsi anavyotakikana kumtunza mumewe na mengine mengi. Mbali na mafunzo msichana husuguliwa liwa na majano mwilini na usoni, haya yakiwa matayarisho ya siku ya harusi.

### **2.2.2 Kupeleka mahari**

Mahari yanapokamilika na mda waliotaka jamaa wa mvulana unapofika, hujiandaa kwa shughuli ya kupeleka mahari kwa familia ya msichana. Siku ya kupeleka mahari huwa ni siku muhimu kwa kuwa familia ya msichana huhitajika kufanya matayarisho ya kuwapokea wageni. Jamaa ya msichana watakuwa wamefanya mandalizi ya kupokea mahari. Vyakula vya aina

mbalimbali huwa vyatayarishwa. Vyakula hivi ni pamoja na matobosha, mikate ya sinia, mikate ya mayai, donasi, mikate ya mofa, nyama choma, samaki wa kupaka, chai nakadhalika.

Mara nyingi shughuli hii hufanywa mshuko wa alasiri Jukumu la kuwapokea wageni huachiwa wajomba na mashangazi. Wao ndio hushughulika katika sherehe hii. Baada ya wageni kupokelewa, huandaliwa vyakula vilivyo tayarisha kwa minajili ya shughuli hiyo. Baada ya kula hutowa kile wameleta. Kama nilivyoeleza hapo awali kuwa mahari huhusisha pesa na funicha, kile hupelekwa huwa ni pesa kwa kuwa fanicha huwekwa kule kwa mvulana mpaka siku ya harusi ndipo msichana ataekewa kwenye nyumba yake. Iwapo mvulana ni mkwasi wa fedha, siku ya kupeleka mahari hupeleka na begi dogo. Begi dogo inamaana ya vyombo kiasi vya msichana ambavyo atatumia akiwa ndani akisubiri siku ya harusi.

Vyombo vinavyowekwa katika begi hili huwa ni lesa kama gora mbili, chupa mbili, mafuta ya mwili, sabuni, kanchiri, viatu vya chooni, tauli, podari na marobu kama mawili. Kama mvulana hana uwezo, basi begi litakuwa lile moja ambalo hupelekwa wakati wa harusi. Mahari yanapotolewa, watu wa familia ya msichana husherehekea kwa kupiga vigelegele na kuimba.

Pesa ile ya mahari huwa ni ya msichana ambaye hutumia kwa maandalizi ya harusi. Hununua mavazi ambayo atavaa wakati huo. Mavazi haya ni rinda la nikaha na la usiku baada ya nikaha, mapambo ya dhahabu na kadhalika. Kama mvulana hana uwezo wa kifedha na kiasi cha pesa za mahari ni kidogo ambacho hakiwezi kugharamia mapambo ya msichana, familia ya msichana hugharamia mavazi ya harusi. Mamake msichana humpa mwanawe dhabu. Hii ndiyo sababu mwanamke wa Kiswahili ni muhimu sana awe na dhahabu hasa akiwa na mtoto wakike.

### 2.2.3 Harusi

Siku mbili kabla ya harusi huwa kuna mapokezi ya wageni na matayarisho ya siku yenyewe. Waswahili ni jamii ambayo huishi pamoja pamoja na mara nyingi huowana kiukoo. Kwa mfano mtoto washangazi na mjomba wanaowana. Kwa sababu hii, sherehe ya harusi hufanywa pamoja. Jamaa wa mvulana na wale wa msichana huchanga kugharamia mahitaji ya shughuli hiyo.

Siku moja kabla ya harusi huwa na matayarisho ya vile vyakula vitakavyopikwa. Vyakula ambavyo hupikwa katika sherehe za harusi huwa ni biriani, pilau na wali mweupe. Matayarisho yake huwa ni kudondolewa kwa mchele, kushambua iliki, vitunguu na kupondwa kwa dawa za pilau. Chakula hiki huwa ni 'limatil harusi' na huliwa baada ya nikaha.

Harusi nyingi siku hizi hufungwa baada ya aduhuri ili nikaha ikishapita watu wajiandae kwa 'lunch', hii ni njia moja ya kupunguza gharama. Nikaha ikifungwa asubuhi, itabidi kuwe na chakula cha kuwalisha waliohudhuria wakiwa wanasubiri sherehe ya mchana 'Lunch'

Siku ile ya harusi asubuhi hutayarishwa rojo la viazi, mahamri na chapati kama kiamsha kinywa. Nikaha hufungishwa msikitini, waliohudhuria kushuhudia hupewa kahawa, na nyama ya kukaanga. Iwapo mskiti uko mbali na nyumbani kwa kinabibi arusi basi itafungwa nyumbani kwao.

Wakati wa harusi, bibi arusi huwa amepambwa kwa mapambo ya kila aina. Hupakwa hina, piko, nywele husetiwa, hupakwa wanja. Kwa ufupi huwa anapendeza. Mara nyingi kwa sababu ya mapambo huwa sura yake inakuwa tofauti na ile ya kila siku. Katika jamii ya Waswahili, msichana haruhusiwi kujipamba na mapambo ya aina yoyote mpaka siku ya harusi yake. Hii ni kwa sababu kama amezoea kujipamba basi hakutakuwa na mabadiliko wakati wa harusi kwa kuwa watu wamemzoea kwa hayo mapambo.



Baada ya ndoa kufungwa, bwana arusi huenda kutoa mkono kwa bibi arusi. Bibi huwa yuko ndani, wakati huu huwa watu wengine hawaruhusiwi kuingia. Bibi arusi hubaki na watu kidogo ambao huwa ni jamaa wake wa karibu. Wakati akitoa mkono, huwa kuna zawadi ya pesa ambayo bwana humpa bibi yake. Huko ndani bwana arusi huwa ameandaliwa vyakula vya aina aina kama vile maji ya maziwa (milkshake) yaliyotayarishwa kwa ustadi kwa ajili yake, sambusa, keki, katilesi, mkate wa sinia, kababu za kobe. Shughuli hii itaenda sambamba na upigaji picha. Baada ya shughuli hii kufikia kikomo, bwana hutoka nje aende kujipumzisha amuache bibi ambaye baadaye atapambwa tena kwa ajili ya sherehe nyingine ya usiku (kupamba).

Shughuli hii ya kutoa mkono huenda sambamba na sherehe ya chakula cha mchana ikiwa ndoa ni ya mshuko wa aduhuri. Kama kuna ukumbi (Hall) karibu, hufanya kwenye ukumbi. Kama hakuna ukumbi banda hutayarishwa na chandarua huwekwa kwenye banda hilo. Waliohudhuria hukusanyika kwenye ukumbi kwa chakula. (lima tul harusi) na vinywaji kama vile soda na maji tamu. Wakati watu wakila, huburudishwa na muziki wa taarab. Mbali na kula wanawake hucheza. Sherehe hii huendelea hadi alasiri. Baada ya sherehe hii, watu hufumukana kuenda kujiandaa kwa sherehe ya kupamba.

Kupamba ni sherehe ambayo hufanywa baada ya nikaha na chakula cha mchana. Huanza baada ya insha hadi saa tano usiku. Mara nyingi shughuli hii hufanywa kwenye ukumbi. Kwenye ukumbi huwa kunatengenezwa jukwaa (stage). Jukwaa hupambwa kwa mapambo tofauti tofauti Bibi arusi naye hurembeshwa tofauti na vile huwa amerembeshwa wakati wa nikaha kwa ajili ya sherehe ya kupamba. Sherehe hii huhudhuriwa na wale waliopewa kadi ya mwaliko. Sherehe huanza baada ya Magharibi ukumbi huwa ushatayarishwa. Huwa na vitumbuizo kama vile taarab. Wale walioalikwa huanza kuingia ukumbini. Wafikapo mlangoni hutakikama kuonyesha

kadi ya mwaliko. Baada ya kutoa kadi, hupewa chakula ambacho huwa kimetayarishwa kwa sababu ya sherehe hii. Chakula hiki huwa kimechangiwa na familia ya bwana na bibi arusi. Chakula kinachotayarishwa hutegemea na idadi ya walioalikwa ndiposa yule hana kadi haruhusiwi kuhudhuria. Kila apewaye chakula huingia kwenye ukumbi na kujitafutia pahali panapomridhisha na kukaa. Pale ndani huwa na vinywaji kama vile soda na maji tamu. Waliohudhuria hula na kunywa huku wakiburudika na muziki wa taarab. Wanawake hucheza.

Mnamo saa mbili usiku, bibi arusi huingia kwenye ukumbi na kukaa kwenye jukwaa. Wakati akiingia, hupigiwa wimbo wake maalumu aupendao ili kumkaribisha kwenye ukumbi. Baada ya mda kidogo, bwana arusi naye huingia ukumbini. Watu hupiga vigelegele kwa furaha na kuwakaribisha maarusi hao. Wakati maarusi wakiingia ukumbini, watu huwa tayari wamekula. Muziki husitishwa na hatua ya sherehe inayofuata huchukua hatamu. Maarusi huwa wamekaa jukwaani, ndugu, jamaa na marafiki waliohudhuria hujitokeza jukwaani kuwazawadi maarusi hao. Shughuli hii huenda sambamba na upigaji picha. Shughuli hii huisha mnamo saa tano usiku.

Baada ya sherehe, maarusi huelekea nyumbani kwao, yaani kwa akina bwana arusi. Chumba cha bwana huwa kimepambwa na fanicha ambayo ni sehemu ya mahari ya bibi arusi. Kila kitu ndani ya chumba kile huwa ni kipya. Vyombo hivi huwa ni kitanda, kabati ya nguo, godoro, zulia, pazia, mashiti na kadhalika. Maarusi hawa hukaribishwa nyumbani kwa vigelegele na wanamake. Huingia chumbani mwao. Chumbani huwa wameandaliwa chakula. Maarusi huwa hawali ukumbini, chakula chao huandaliwa chumbani, nyumbani kwa bwana arusi vyakula wanavyoandaliwa huwa katilesi, maji ya maziwa, sambusa, kababu, keki na kadhalika.

Wakishamaliza kula, watu waliokuwa chumbani hutoka nje na kuwaacha maarusi hao. Huu ndio wakati maarusi hawa hutekeleza kitendo cha kujamiana, hali jamaa wa bawana na bibi

arusi wakiwa nje wakisubiri majibu, yaana kama bibi arusi ni mwanamwali (bikira) au la hali hii itadhihirika kupitia shiti iliyotandikwa kitandani. Kama bibi arusi ni mwanamwali basi shiti itakua na doa. Kama msichana alikuwa bikira, watu hasa wanamake hupiga vigelegele na kuimba ishara ya kufurahia kwa kuwa walifanikiwa kumtunza msichana wao hasa jamaa ya bibi arusi.

Nikaha inapofungwa na sherehe zote kuisha, bibi arusi hukaa ndani, ya nyumba yake siku saba. Baada ya siku saba kuisha, familia ya bwana huandaa sherehe ndogo ya kumtoa nje. Bibi arusi anapomaliza siku saba na kutolewa nje, huandamana na mumewe kuenda kwa wazazi wake kusalimia.

### **2.3 Hitimisho**

Katika sura hii tumeangazia utaratbu wa ndoa na harusi katika jamii ya Wadigo na Waswahili, katika jamii ya Wadigo utaratibu huu unahusisha posa, kupeleka mizigo, matayarisho ya harusi na mwisho harusi. Nao waswahili utaratibu wao ni posa, kupeleka mahari na mwisho harusi.

## **SURA YA TATU**

### **NYIMBO ZA HARUSI**

#### **3.0 UTANGULIZI**

Katika sura hii tutashughulikia nyimbo za harusi katika jamii ya Wadigo na Jamii ya Waswahili, katika nyimbo hizi tutajikita katika kipengele cha maudhui yaani mawazo yanayodhihirika katika nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili.

Mbali na maudhui, tutashughulikia majukumu yanayotekelezwa na nyimbo hizi katika jamii baada ya kushughulikia maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi katika jamii hizi mbili, kwa kuwa ni jamii mbili tofauti zenye utamaduni tofauti, tutalinganisha na kutofautisha. Nyimbo zitakazo shughulikiwa ni za kiasili na za bendi ya taarab. Kwa kuwa jamii zote mbili hupigisha taarab katika sherehe zao za harusi, wakati tukishughulikia nyimbo hizi tutaangazia maudhui na majukumu bila kulinganisha wala kutofautisha kwa kuwa ni hizo moja katika jamii zote mbili. Mbali na maudhui na majukumu yanayotekelezwa na nyimbo hizi , pia tutaangazia wanaolengwa na ujumbe wa nyimbo hizi katika jamii.

#### **3.1 Nyimbo Za Kiasili**

##### **3.1.1 Nyimbo za harusi za Wadigo**

Katika jamii ya Wadigo sherehe za harusi hufuata utaratibu maalumu, nyimbo nazo hutegemea utaratibu huo. Hii ni kwa sababu wimbo hutegemea shughuli inayotendeka katika utaratibu mzima wa harusi. Mara nyingi nyimbo za harusi huangazia hali halisi inayodhihirika katika jamii ya maarusi.

### **3.1.2 Maudhui**

Kwa mujibu wa Kimani na Rocha (1999), maudhui ni ujumbe wajumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi, iwe riwaya, tamthilia, shairi au wimbo. Maudhui ni sehemu ya maana na huingiliana na mada. Ni katika maingiliano baina ya mada na maudhui ambapo ukweli uliokusudiwa hujitokeza. Kulingana na Wamitila (2003) maudhui ni yaliyomo au jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi yoyote. Katika sehemu hii tunashughulikia masuala yanayozungumziwa katika nyimbo za harusi za Wadigo.

### **3.1.3 Maombi**

Katika jamii ya Wadigo, wanaamini ya kwamba, kabla ya kufanya jambo au shughuli yoyote, kuna umuhimu wa kutanguliza maombi ili Mwenyezi Mungu ailinde shughuli hiyo iwe niyenye kutendeka kwa usalama. Wakati msafara wa bwana arusi ukianza safari kuelekea kwa bibi arusi kwenda kuo, kuna wimbo ambao huimbwa ambao huwa ni maombi ili shughuli ya kuenda kuowa iwe niyenye usalama.

Katika wimbo huo huwa wanamuomba Mwenyezi Mungu waende safari yao salama bila shida yoyote njiani, sherehe ya nikaha ikafanyike bila tatizo lolote tena wakati wakirudi nyumbani pamoja na bibi arusi, safari iwe niyenye usalama. Hii ni kwa sababu sherehe hizi huwa na nuksi mara nyingi. Gari iliyobeba msafara wakati mwingine huhusika katika ajali. Katika jamii ya Wadigo kuna imani kwamba katika hali halisi binadamu hafurahii mazuri au mafanikio ya mwenzake. Wakati mtu akiandaa harusi ya mtoto wake, mahasidi huhusudu shughuli hiyo ili isiwe niyenye kufana. Hali hii ndiyo hufanya watu kutanguliza maombi kwanza ili Maulana aepushe husuda hizo.

### **3.1.4 Umuhimu wa kuowa mbali**

Kuna wimbo ambao unazungumzia kuhusu kuowa mbali, kwamba wakati mtu anapooa mbali na kwao hujua siri za kule anakooa. Kuoja mbali inamaana mbili tofauti.

Kwanza ina maana ya umbali wa kimaeneo, pia ina maana ya kuoja katika jamii tofauti na ile unayotoka.

Vijana katika jamii ya Wadigo huhimizwa kuoja kutoka maeneo ya mbali na kwao. Pia huhimizwa kuoja kutoka jamii zingine, kutokana na hali hii vijana wanajifunza mambo mengi kutoka kule wameoa ambayo hayapatikani katika jamii yao. Mbali na kujifunza mambo, pia hufahamu utamaduni wa jamii ambayo ashaoa. Katika kila jamii kuna mambo ambayo ni ya ndani na hujulikana na wanajamii wenyewe. Kijana anapooa katika jamii hiyo huchukuliwa kama mmoja wa wanajamii na ndiyo huhusishwa katika mambo hayo ya ndani ya jamii husika.

Katika jamii ya Wadigo, wanaamini ya kwamba wakati kijana wao anapooa au kuolewa katika jamii nyingine, ni njia moja ya kukuza jamii. Hii ni kwa sababu baada ya ndoa jamii zile mbili yaani ya bwana na bibi arusi huwa zimeungana na kuwa jamii moja, kukiwa na shughuli ya kutekeleza, huungana na ile nyingine kufanya shughuli hiyo.

### **3.1.5 Msamaha**

Katika maisha ya kila siku binadamu hutangamana na wengine. Katika harakati na maingiliano na wengine, mtu hujikuta katika makosa wakati mwingine bila hata kukusudia. Binadamu ni kiumbe mwenye kuhifadhi matendo hasa mabaya. Jambo lolote baya linapotokea hubaki katika fikra za waja miaka nenda miaka rudi. Wakati mwingine makosa haya huhusishwa na mtu binafsi au familia kwa jumla. Wakati familia wanapotaka kuoza msichana wao, kabla ya ndoa familia ya mvulana hufanya uchunguzi wa tabia na mienendo ya msichana huyo.

Uchunguzi huu hufanywa kupitia majirani. Huu ndio wakati siri nyingi kuhusu familia ya msichana hujulikana. Familia ya msichana hasa wazazi wake, wanapogundua ya kwamba siri ishajulikana huomba msamaha kwamba yaliyopita yashapita wanaomba wasamehewe kwa makosa waliokosa na shughuli ya ndoa ifanywe kwa usalama bila tatizo au kikwazo chochote. Hali hii ya kuomba msamaha na kutaka shughuli ya ndoa kufanywa kwa usalama huwasilishwa kupitia wimbo wakati wa sherehe za harusi.

### **3.1.6 Uvivu**

Hii ni hali ya mtu kutofanya au kufanya jambo kwa ulegevu. Hali hii husababishwa na uchovu wa mwili au kutokuwa na hisia au hamu ya kufanya jambo hilo. Katika jamii ya Wadigo, mwanamke huchukuliwa mtunzaji wa nyumba. Hudumisha usafi wa nyumba, kama vile kufagia, kufua, kuosha vyombo na pia shughuli za upishi. Wakati mamavyaa anapopata makazamwana, huwa na matarajio ya kupumzika kutekeleza shughuli hizi. Mkazamwana ndiye hushika usukani wa kutunza boma naye mamavyaa hupumzika. Hufanya tu kazi ndogo ndogo kumsaidia mkazamwanawe.

Wakati mwingine mambo huenda kinyume na matarajio ya kila mwanajamii. Mkazamwana hushindwa kutekeleza majukumu yake ya kutunza boma na badala yake humuachia mamakevya kazi zote. Hali hii humfanya mamake bwana arusi aanze kumlaumu mamake bibi arusi kwa kushindwa kumfunza binti yake kazi za nyumbani.

Ujumbe huu unapitishwa kupitia wimbo ambapo mamake mvulana anamlaumu mamake msichana kwamba alimpa maganda ambayo hayamsaidii, shida ya kazi za nyumbani bado angalinayo.

### **3.1.7 Ukosefu wa wajibikaji**

Jukumu la kumlea mtoto wa kike ni la mama. Katika harakati ya kumlea bintiye, mama anatakikana kumfunza mwanawe kazi za nyumbani kama vile kupika mapishi tofutti tofauti, kufua, kuosha vyombo, kupamba nyumba na kadhalika. Wakati mwingine mama anashindwa kutekeleza wajibu wake wa kumfunza binti yake kazi za nyumbani. Hali hii hutokea pale mama hana mda wa kukaa na msichana wake na kumfunza kazi. Hali hii ni kwa kuwa labda ameajiriwa na ninadra sana kupatikana nyumbani. Kazi za nyumbani ameziachia mfanyikazi ambaye amemuajiri au wakati mwingine msichana huwa yuko masomoni kwa kipindi kirefu na huja tu kwa mda mchache nyumbani.

Matatizo haya hudhihirika wakati msichana anaposhindwa kufanya kazi hizo anapopata jiko lake. Hali hii inafanya mamake msichana alaumiwe na chivyere wake wa kike kwamba alikosa kuwajibika katika malezi ya bintiye na sasa amempa maganda ambayo hayana msaada wowote.

### **3.1.8 Majukumu ya bwana**

Katika ulimwengu halisi bwana ndiye kiongozi katika familia. Kwa kuwa yeye ndiye kiongozi, ana majukumu anayohitajika kuyatekeleza. Ni wajibu wake kuhakikisha familia inapata mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, matibabu, mavazi, elimu na kadhalika, kwa kuwa bwana arusi ndiyo mwanzo anatoka katika ujana na kuingia katika uzee, kuna haja ya kuhamasishwa kuhusu majukumu yake kama kiongozi wa familia. Kabla ya kuoia alikuwa akifanyiwa kila jambo na wazazi wake, lakini sasa amepata jiko ni lazima ajiandae kushughulikia jiko hilo. Baada ya harusi watu katika familia huwa ni bwana na bibi yake, huwa hawajapata watoto. Majukumu ya bwana kwa mda huu huwa ni kuangalia mahitaji ya bibi yake.



Wanawake kutoka familia ya bibi harusi huimba wimbo kumueleza bwana arusi wajibu wake kwa mkewe ambaye bado ni kijana.

*Bwana arusi asomerwe baruwaye*

*Namupha mwana*

*Mwana ni barubaru*

*Usimuphe tenge wala usiphuphe gushe*

*Mukatire lesa na siliki wee*

*Mwenye abwambwarise*

### **Tafsiri**

Bwana arusi asomewe barua yake

Nampa mtoto

Mtoto ni kijana

Usimnunulie tenge wala kaniki

Mnunulie lesa na siliki

Mwenyewe aringe.

Bwana arusi anaambiwa kwamba bibi arusi bado ni kijana anahitaji kurembeshwa kwa mapambo. Amnunulie nguo nzuri zenye kupendeza kama vile lesa na siliki na wala sio kaniki na tenge. Katika jamii ya Wadigo matenge na kaniki huchukuliwa kuwa mavazi ya wanawake wazee.

### **3.1.9 Wivu**

Kwa mujibu wa kamusi ya karne ya 21, (2014) neno wivu lina maana mbili. Kwanza ni hali ya kuwa na kinyongo au kijicho wakati mtu anapopata mali, mafanikio au maendeleo ya mtu mwingine. Maana ya pili ni tabia ya mtu kusononeka aonapo mpenzi wake ana uhusiano wa kimapenzi na mtu mwingine.

Katika muktadha huu tunazungumzia maana ya pili ya neno wivu. Katika mazingira halisi hakuna mwanamka anayependa mumewe aoe mke wa pili. Licha ya kwamba imani ya dini ya kiislamu inaruhusu mwanamume kuoa wake wawili hadi wanne, wanawake wakiislamu hawafurahii hali hii, hukubali shingo upande kwa kuwa ni kati ya sunna za mtume.

Hali inayowafanya wanawake wachukie uke wenza ni kwamba bwana huhitajika kugawa penzi lake kwa wake aliowaoa sawa sawa bila kubagua hali ambayo haiwezekani.

Kwa vyovyote vile, bwana huegemeza penzi lake kwa mmoja wao na yule mwingine penzi hupungua. Kwa sababu ya kuhofia hali hii, mwanamke akimuona bwanake anaanza kuwa na fikra za kuoa bibi wa pili, hufanya kila hila hata kuenda kwa wachawi kumroga mumewe asifikirie kuoa mke mwingine.

*Mharusi mzima*

*Wagwira na kuku mwiru*

*Aya lagulwa*

*Gwinyo gwinyo*

*Anaphiha mzungani*

*Akaloge mlumewe mwenye*

*Asihale mchetu wa phiri*

## **Tafsiri**

Bibi arusi

Alishikwa na kuku mweusi

Anaenda kwa mtibabu

Gwinyo gwinyo

Anaenda mzunguni

Akamroge bwanake

Asiowe mke wa pili

### **3.1.10 Ushirikina**

Hii ni tabia ya kuamini mambo ya uganga na uchawi.

Wakati mwingine binadamu hufikwa na shida, katika hali hii huona kwamba njia ya pekee na haraka kutatua shida hiyo, nikuenda kwa mganga au mchawi.

Mwanamke huchukulia kuwa kupata mkemwenza ni sawa na kukaribisha shida ndani ya nyumba. Kulingana na mwanamke njia ya haraka ya kuepuka shida ya aina hii ni kuenda kwa mchawi afanyiwe mambo ambayo yatamzuzua bwanake hata asiwe na fikra za kuoia mke mwingine.

*Mharusi mzima*

*Wagwira na kuku mwiru*

*Aya lagulwa*

*Gwinyo gwinyo*

*Anaphiha mzungu*

*Akaloge mlumeye mwenye*

#### **Tafsiri**

Bibi arusi

Alishikwa na kuku mweusi

Anaenda kwa mtibabu

Gwinyo gwinyo

Anaenda mzungu

Akamroge bwanake

### **3.1.11 Umbeya**

Umbeya ni tabia ya kutoa habari bila ya kutumwa au kuulizwa. Katika jamii kuna watu ambao huropokwa kusema ya wenziwao hasa wakijua kuwa habari hizo si nzuri na huenda zikamwaibisha anayehusika iwapo zitajulikana na watu wengine.

Hali hii husababisha ugomvi katika jamii. Iwapo anayesemwa atafikiwa na habari hizo na yule anayeeneza habari hizo basi huteta na yule mwenye kueneza habari hizo. Mbali na ugomvi, tabia ya umbeya huvunja uhusiano katika jamii. Kitendo hiki kinakashifiwa kupitia wimbo.

Wakati mwingine yanayoenezwa huwa ni mambo ya kweli, lakini kwa sababu kujulikana kwake kuna sababisha ugomvi, aibu na madhara mengi, mambo mengine yanafaa kuhifadhiwa kama siri ili kuepuka madhara yake.

*Avi mwamba mnarora*

*Rorani vinono*

*Msibanange kaya yehu na umbeya.*

*Mwi mrorwao mna umbeya*

### **Tafsiri**

MLISEMA MNAOA

Oweni vizuri

Msiharibu mji wetu na umbeya

Nyinyi manaolewa ni wambeya.

### **3.1.12 Tamaa na ubinafsi**

Tama ni hali ya kutaka sana kitu, ubinafsi nao ni tabia ya mtu kujali maslahi yake mwenyewe na kupuuza ya wengine. Maneno haya mawili yanaenda pamoja kwamba mtu akiwa na hamu ya kitu, hung'ang'ana na katika hali hii huwa hajali hali au maslahi ya wengine. Katika jamii ya Wadigo msichana anapochumbiwa, wazazi wake hupewa ada fulani ya pesa kama shukrani kwa kumzaa na kumlea binti anayetaka kuolewa. Pesa zile hugawanywa, baba akapewa zake na mama kupewa kiasi fulani cha fedha hizo.

Wakati msichana anaenda kwake kuanza maisha ya ndoa, kuna haja ya wazazi kumnunulia baadhi ya vyombo vya nyumbani kama zawadi vya kuanzia maisha. Jambo hili

wakati mwingine hupuuzwa na baadhi ya wazazi. Hali hii hutokea pale mzazi anaingiwa na tamaa ya pesa ambapo hufikiri anapochukua kiasi fulani cha fedha kwa lengo la kumnunulia bintiye vyombo huenda zikapungua na ashindwe kufanya mahitaji yake mengine. Kupitia fikra hizi tunaona mzazi anakuwa mbinafsi kwa kujali shida zake na kupuuza mahitaji ya mtoto wake.

*Kuna baba kassimu*

*Wagwira maganage*

*Achika mfukoni*

*Mwari kayafungulwa*

*Chivyere mwayangu anawaibu*

### **Tafsiri**

Kuna mzee kassimu

Alichukua mamia yake

Akaeka mfukoni

Bibi arusi hakuzawadiwa

Chivyere mwenzangu anaibu

### **3.1.13 Umoja na ushirikiano**

Jamii mbili zenye asili na utamaduni tofauti huungana, wakabadilishana utamaduni, wakashirikiana na kufanya mambo yao kwa pamoja. Hali hii husababishwa na ndoa baina ya watu kutoka jamii tofauti. Kabla ya ndoa huwa hakuna uhusiano wowote ule, lakini baada ya kuowana huwa watu wanahusiana na kuwa kitu kimoja. Shughuli zao hufanya pamoja kwa ushirikiano kama jamii moja.

Ndoa huleta mshikamano baina ya watu kutoka jamii tofauti.

*Mduruma na mdigo*

*Rero andagwirana*

*Rero andagwirana*

*Mayo wee naphiha*  
*Golini nikalole mwanangwa*  
*Anangwa ahenda vyalika*  
*Chivyere wee unaphaya phaya*  
*Mduruma na mdigo*  
*Rero andagwirana*

### **Tafsiri**

Mduruma na mdigo  
Leo watashikana  
Leo watashikana  
Mama yangu naenda  
Golini nikaowe watoto wa wenyewe  
Watoto wa wenyewe wanapendeza  
Chivyere unamchezo  
Mduruma na mdigo  
Leo watashikana

### **3.2 Majukumu**

Watafiti wengi wa kiafrika wanakubali kwamba nyimbo zina nafasi muhimu katika jamii kama anavyosema Wamitila (2003), Takriban shughuli zote za binadamu kama kulima, kusuka, kuoja, kulea, kufariji, kuliwaza na kuzika, huandamana na nyimbo na vimbaji.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), ndoa ni sherehe muhimu ya kitamaduni katika jamii, sherehe hii huandamana na kila aina ya tafrija zikiwepo nyimbo. Ingawa kimsingi nyimbo hizi huandamana na sherehe za ndoa, majukumu yake ya ziada hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Katika sehemu hii tutaangazia majukumu ya nyimbo za harusi za kiasili katika jamii ya Wadigo. Kwa kuwa nyimbo za harusi ni nyingi, tutaangazia majukumu yanayojitokeza katika nyimbo tulizoziteuwa kwa ajili ya utafiti huu.

### **3.2.1 Kuhifadhi**

Katika jamii ya Wadigo kuna nyimbo ambazo huimbwa katika sherehe za harusi ambazo ni za maombi. Jamaa wa maarusi wanaomba ili shughuli za harusi ziendeshe kwa usalama, kwa namna hii nyimbo hizi zinatekeleza jukumu la kuhifadhi mila, desturi na itikadi za jamii ya Wadigo kwamba kabla ya kuanza safari, kuna haja ya kuelekea kwa Maulana kwa maombi ili shughuli hiyo isipatwe na matatizo.

Pia kuna hali ya kuendeleza imani ya jamii ya Wadigo kwamba katika jamii huwa na mahasidi ambao hawafurahii mafanikio ya wengine, huenda juu chini kuhusudu jitihada za wenzao ili wasifanikiwe.

Kuna jukumu la kijitakasa kwamba wakati mwingine mtu hufanya makosa bila hata kukusudia. Ukishagundua makosa uliyoyatenda, kuna haja ya kuomba msamaha ili uweze kushirikiana na wengine.

*Salama wee navyoya salama*

*Samahani wee navoya salama*

*Salama wee ukaowe salama*

*Salama wee uye salama*

#### **Tafsiri**

Salama naomba salama

Samahani naomba salama

Salama tukaowe salama

Salama turudi salama.

### **3.2.2 Kuhimiza**

Baadhi ya nyimbo za harusi katika jamii ya Wadigo hutekeleza jukumu la kuhimiza mambo au matendo muhimu katika jamii. Vijana wanahimizwa kuoa katika jamii zingine tofauti na yao.

Wakati mtu anaoa kutoka jamii nyingine, hujua utamaduni au mambo ya ndani kuhusu jamii hiyo. Pia msichana anapoolewa katika jamii tofauti na ile yake, hufahamu na kujifunza utamaduni wa jamii hiyo.

*Kulola kure ni kumanya siri za atuu.*

### **Tafsiri**

Kuoa mbali ni kujua siri za watu.

Wazazi wanahimizwa kutekeleza majukumu yao kama walezi hasa wamama. Wanawake ndio hushughulika katika kulea watoto. Yeye ndiye huwafunza kazi hasa za nyumbani. Iwapo mama hatatekeleza majukumu hasa kumfunza kazi msichana wake ataenda kulaumiwa na mamake mvulana wakati msichana wake atashindwa kufanya kazi kule atakakoolewa.

*Chivyere waniphani myao*

*Waniphani myao*

*Wanipha maphephe*

*Kuni nitphiye mwenye*

*Mkazamwana anarora*

*Madzi niphaye mwenye*

*Mkaza mwana anarora*



## **Tafsiri**

Chivyere ulinipa nini mwenzio

Ulinipa nini mwenzio

Ulinipa maganda

Kunini niende mwenyewe

Mkazamwana anangalia

Maji nikateke mwenyewe

Mkazamwana anangalia

Pia kuna wimbo unaotekeleza jukumu la kuhimiza umoja na ushirikiano, huhimiza jamii kupitia kitendo cha ndoa.

*Chivyere wee unaphaya phaya*

*Mduruma na mdigo*

*Rero andagwirana*

*Chivyere unacheza*

*Mduruma na mdigo*

*Leo watashikana*

### **3.2.3 Kukashifu**

Katika jamii kuna watu wenye tabia ambazo zinaenda kinyume na maadili ya jamii. Tabia hizi ni kama vile uvivu, wivu, ushirikina, umbeya, tamaa, ubinafsi na kadhalika. Vitendo hivi husababisha madhara katika jamii kama vile kugonganisha watu, kuvunja ndoa za watu, kudhulumu wengine na kutojali maslahi ya wengine. Kwa sababu ya madhara haya kuna haja ya kukashifu vitendo hivi, katika jamii kuna nyimbo zinazotekeleza jukumu hili la kukashifu vitendo hivi.

*Kuni niphiye mwenye*

*Madzi niphiye mwenye*

*Vyombo nisuwe mwenye*

*Kuphyera ni phyere mwenye*

*Kubiya nibiye mwenye*  
*Mkaza mwana anarora*

### **Tafsiri**

Kunini niende mwenyewe  
Maji nikateke mwenyewe  
Vyombo nioshe mwenyewe  
Kufagia nifagie mwenyewe  
Kupika nipike mwenyewe  
Mkaza mwana anangalia

### **3.2.4 Kuhamasisha**

Wakati mwingine vijana wa kiume hujiingiza katika maisha ya ndoa bila hata kuwa na ufahamu wa majukumu yao katika ndoa.

Hali hii husababisha talaka, kuna wimbo ambayo unatekeleza jukumu la kuhamasisha vijana wa kiume kuhusu majukumu yao wanapoingia katika maisha ya ndoa.

Ni wajibu wao kuwatunza wakezao pindi wanapooa. Ni jukumu lao kuwanunulia nguo ambazo zapendeza na mapambo mengine. Kuna haja ya kuhamasishwa kwani wamezoea kutendewa mambo na wazazi wao kabla ya kuo. Huenda wakadhani kwamba hata baada ya kujiingiza katika ndoa, wazazi watawafanyia pamoja na wake wao.

*Bwana arusi asomerwe baruwaye*  
*Nnamupha mwana*  
*Mwanani barubaru*  
*Usiphu tenge wala usimuphe gushe*  
*Mukatire lesa na siliki wee*  
*Mwenye ambwambwarise.*

## **Tafsiri**

Bwana arusi asomewe barua yake

Nampa mtoto

Mtoto ni kijana

Usimpe tenge wala usimpe kaniki

Mkatie lesa na siliki

Mwenyewe aringe.

### **3.3 Walengwa Wa Ujumbe**

Ujumbe unaodhihirika katika nyimbo za kiasili za harusi za Wadigo ni maarusi na jamaa wao wa karibu. Bwana arusi na wazazi wake. Ujumbe huu huwa unatoka kwa wanajamii ukielekezwa kwao. Nyimbo hizi huimbwa wakati wa sherehe za harusi kama njia moja ya kutumbuiza na kuburudisha maarusi na waliohudhuria sherehe hiyo.

Mambo yanayo angaziwa katika nyimbo hizi si kwamba maarusi au jamaa zao wameyatenda la hasha, lakini huwa wanapewa tahadhari iwapo wana nia ya kuyatenda, wasiyatende. Haya huwa ni yale mabaya ambayo hayambatani na maadili ya kijamii kama vile bibi arusi kumroga mumewe. Wakati mwingine ni njia moja ya kumueleza bwana arusi majukumu yake kama kiongozi wa nyumba. Mbali na maarusi na familia zao, wanajamii wengine pia huhamasishwa kuhusu maisha ya ndoa na matendo ambayo hayakubaliki katika jamii.

### **3.4 Nyimbo Za Harusi Za Waswahili**

#### **3.4.1 Maudhui**

##### **3.4.1.1 Maombi**

Kama tulivyosema hapo awali kwamba Waswahili ni wafuasi wa dini ya Kiislamu, kama itikadi ya dini ya kiislamu kila jambo mtu anataka kufanya lazima aanze kwa maombi. Hali hii

inajitokeza hadi kwa nyimbo za harusi, kunazo zinazoanza kwa maombi na nyingine maombi yanadhihirika katikati ya wimbo.

*Ya Rabbi, takabalie dua*

*Allahu ya rabba ilahi wahida*

*Bwana hako bwana hako*

*Wendee kuswali isha*

Mistari hii imetoka katika nyimbo tatu tofauti, mwimbaji anamuomba Mwenyezi Mungu akubali dua zao kwa kujibu matakwa yao. Pia mwimbaji analeta dhana ya kuhudhuria swala ya isha ambayo husaliwa saa mbili usiku.

### **3.4.2 Mapenzi**

Mapenzi hudhihirika pale wawili wanapopendana. Ndoa huja baada ya wawili kupendana na kusafiana nia na kuamua kuishi pamoja kama bibi na bwana. Mapenzi haya hudhihirika kupitia vitendo wanavyofanya wawili hawa.

Kuna baaadhi ya nyimbo ambazo hudokeza kuhusu vitendo hivi vya kimapenzi.

*Ukombali ukombali kikupenda kutojua*

*Huninyua huninyua kichandani niyele*

*Hatutoki hatutoki mpaka tupigane kisi*

Mwimbaji anamwambia mpenzi wake kuwa ako mbali akimhitaji hatajua. Anaendelea kusema kuwa, mpenzi wake humuinua akamueka kitandani alale. Pia anasema ya kwamba wakati wakiachana kuenda kwa shughuli mbalimbali hupigana kisi mwanzo ndipo waende wanakoenda ishara ya mapenzi baina yao.

### 3.4.3 Unafiki

Katika jamii kuna watu ambao hujifanya ni wazuri lakini nia yao ni kumtafuta mtu undani wake kisha baadaye wakaeneza mambo yake mtaani. Mara nyingi hutafuta yale mabaya ambayo mja yuko nayo na hatimaye kuyaeneza ili kumuaibisha muhusika.

Baadhi ya nyimbo za harusi huangazia tabia hii.

*Wala hakuna rafiki eee hae wakusafiana nia*

*Hawa ndiyo kina panya ee hae*

*Huuma wakivuzia*

Mwimbaji anatoa tahadhari kwamba hakuna rafiki ambaye waweza kumsafia nia kwa kumwambia siri zako kwa sababu atachukua siri zile akaeneze mtaani. Amewafananisha na panya ambao huuma na kivuzia.

### 3.4.4 Vijembe

Hii ni hali ya wanawake kurushiana maneno ambayo yamejaa matusi, kejeli na bezo wakiwa na nia ya kuudhiana. Mara nyingi hali hii hutokea pale wanawake wamepokonyana mabwana. Wakati mwingi huwa baina ya mwanamke muhuni na aliyeolewa. Wakati mwingine bwana anaanza uhusiano na mwanamke muhuni, bibi yake akishagundua huanza kuteta baadaye hurushiwa vijembe na yule hawara wa mumewe.

Kuna baadhi ya nyimbo ambazo hudhihirisha ukweli huu.

*Mzuie mumeo, sikuja kumwita*

*Sikufanya tanzi, kaja kamkota*

*Alipiga hodi, kamwambia pita*

Hawara anamwambia amzuie mumewe kwa kuwa hakumwita, bwana mwenyewe ndiye aliyetaka uhusiano naye, naye akamkubalia.

### 3.4.5 Pongezi/Kusifu

Kuna baadhi ya nyimbo ambazo bibi anampongeza au kumsifu mumewe.

Sifa hizi zaweza kuwa ni za kimaumbile, yaani jinsi alivoumbwa, mwendo wake, kazi anayofanya au bidii aliyonayo wakati akitekeleza jambo fulani.

Nihatia katika jamii ya Waswahili mwanamke kumkashifu au kumsengenya mumewe mbele ya wanawake wengine. Hata kama hakuna uhusiano mzuri baina yenu, si vyema kutoa siri za mumeo au kasoro zake kwa watu wengine.

*Bosi langu bosu langu hufanya kazi ofisi*

*Mwendo wake mwendo wake heunda kama tausi*

*Nimepata dereva ajuae gari yangu yeenda mbio*

Mistari hii inadhihirisha ukweli kwamba mwanamke humpongeza yule mume aliye muoa.

### 3.4.6 Majuto

Wawili wapendanapo huona maisha ni mazuri hadi wakamua kuishi pamoja ili waendeleo kufurahia mapenzi yao kama bibi na bwana wala sio marafiki tu.

Baada ya harusi na kuishi kwa mda fulani maisha hubadili mkondo mwingine ambao ni tofauti na ule wa maisha ya awali. Upendo ule wa awali hupungua kadri vile siku zinavyozidi kuongezeka. Mara nyingi penzi la bwana kwa mkewe ndilo huanza kupungua.

*Pendo la awali la zama za tangu*

*Hakika umelibadili, liko kwa mwenzangu*

*Kwa hivyo himili, farikano langu*

Jamii ya Waswahili ni waislamu, wanaruhusiwa kuoza zaidi ya bibi mmoja. Hapa mwimbaji anamwambia mumewe kuwa pendo la zamani amelibadili na kulipeleka kwa mke mwingine. Bibi wa kwanza anajuta kwani hakujua kuwa mumewe angeoa mke mwingine siku za usoni.

### **3.4.7 Majukumu Ya Bwana**

Bwana kama kichwa katika nyumba huwa na majukumu ya kutekeleza. Moja wapo kati ya majukumu hayo ni ulezi.

Ulezi unajitokeza pale anahitajika kununua chakula, nguo, mavazi na kadhalika.

Kwa kuwa jamii ya Waswahili wanaishi mwambao wa Pwani, wengi hujishughulisha na uvuvi kama njia moja ya kujikimu katika maisha yao na jamaa wao.

*Wanao walia ndege*

*Wee leo mwandege*

*Wanao walia*

*Ukenda pwani*

*Wania kuwaia*

*Wanao walia*

Mwimbaji anamtahadharisha bwana arusi kwamba akienda pwani kuvua samaki basi asikawie arudi nyumbani kuangalia mahitaji ya jamii yake kwani watoto wake huenda wakalia kwa sababu ya kukosa chakula.

### **3.4.8 Mapishi**

Waswahili wanajulikana kwa mapishi ya aina mbalimbali kama vile pilau, biriani, vitumbua, mkate wa sinia, mchuzi wa nazi na kadhalika. Wamebobeza katika mambo ya upishi. Katika jamii ya Waswahili, wakati mtu yuataka kuoja, hangalii uzuri wa mke anayetaka kumuowa lakini huangalia mapishi.

Je anaweza kupika, na sio kupika tu bali kupika vyakula tamu.

Kuna nyimbo zinazoangazia kuhusu baadhi ya mapishi katika jamii ya Waswahili.

*Nipeni wino mweusi, niwasifie kipungu*  
*Kwa uzuriwe halisi, mtamu asotewengu*  
*Mwanzo mpate nasima, alafu na kachumbari*  
*Nikikupa la zaidi, umtiye kwa mtuzi*  
*Hakika utafaidi, haswa ukiwa wa nazi*

Mwimbaji anasifu kitoweo cha kipungu ambaye huweza kutayarishiwa kachumbari au apikwe kwa mchuzi wa nazi. Kipungu ni aina ya samaki anayepatikana katika bahari hindi. Ako katika familia moja na papa.

### **3.4.9 Uasherati**

Jamii wakati mwingine hujihusisha na vitendo viovu kama vile uasherati ambao huwa ni kinyume na maadili ya jamii. Hali hii hujitokeza kwa namna mbili. Kwanza huweza kuwa baina ya mke na mume ambao hawajaoa au kuolewa. Kwa namna nyingine huwa baina ya mume aliyeowa na mke ambaye hakuolewa.

Hali inayo zungumziwa katika nyimbo za harusi za Waswahili huwa ni ile ya bwana aliyeowa na mke ambaye hakuolewa.

Mistari ifuatayo inadhihirisha ukweli huu.

*Mzuie mumeo, sikuja kumwita*  
*Sikufanya tanzi, kaja kamkota*  
*Alipiga hodi, kamwambia pita*

Hawara anamwambia amzuie mumewe kwa kuwa hakumwita, bwana mwenyewe ndiye aliyetaka uhusiano naye, naye akamkubalia.



### **3.4.10 Madhara Ya Kupenda**

Kuna baadhi ya waja ambao wanapopenda hupenda kabisa bila hata kudhania kwamba huenda mambo yakaenda kombo na uhusiano huo ukakatika na kutakikana kuchukua hatua nyingine yakutafuta mapenzi pahali pengine. Hali kama hii humfanya mtu achukie wanaume au wanawake wote na abaki bila mpenzi katika maisha yake yote. Kupenda si kubaya lakini kuna haja ya kuwa na mipaka katika hali ya kupenda. Hii ni kwa sababu wakati penzi limehama pahali lilikuwa basi kusiwe na madhara yoyote, maisha yaenda kama kawaida.

Hali hii wakati mwingine husababisha maafa kwa aliyeachwa. Hii ni kwa sababu hakudhani jambo kama hilo laweza kutokea, hakuwa amejiandaa kwa hali kama hiyo kumfika.

*Yaa laitani, nilifahamu awali*

*Ndani moyoni, nisingekuweka asili*

*Kwani hufaeni, moyo si ramli*

*Nimeenda digo, njia za hatari*

*Si kucha milima, wala bahari*

*Moyo wakupenda, hauna nadhari*

Mshairi anasema kwamba laiti angejua hangemueka moyoni mpenzi wake, lakini moyo wa binadamu si ramli kwamba utatambua yale ambayo yatatokea baadaye. Anaendelea kusema kuwa ameenda digo kwenye njia za hatari lakini hakujali hatari hiyo kwa kuwa alikuwa amependa na kila moyo wakupenda hauna tahadhari.

### **3.5 Majukumu**

Nyimbo za kiasili za harusi za Waswahili, zinatekeleza majukumu mbalimbali katika jamii. Katika jamii kuna mambo kadha wa kadha ambayo yanatendwa na baadhi ya wanajamii.

Kunayo ambayo ni mfano mzuri kwa wanajamii wengine na yanastahili kuigwa. Pia kuna matendo mengine hayambatani na maadili ya jamii, haya hayafai kuigwa na wanajamii. Nyimbo za harusi zinatoa mtazamo na mwelekeo kuhusu mambo hayo.

### **3.5.1 Kuhimiza**

Kama tulivyosema kuna baadhi ya nyimbo ambazo huanza kwa maombi au yanapatikana katikati ya nyimbo hizo. Hali hii inaonyesha umuhimu wa maombi kwamba waja wana himizwa kuanza shughuli zao kwa maombi ili Mungu awaongoze katika kufanikisha shughuli hizo. Kuna baaadhi ya nyimbo zinazo gusia swala za faradhi, nyimbo hizi zinahimiza umuhimu wa mja kumuabudu Mola wake kama alivyoamrisha.

Mbali na maombi kuna nyimbo zinazo himiza matendo mazuri yanayoleta mapenzi baina ya wapendanao. Waja wanahimizwa kuiga matando hayo ili kuyafanya mapenzi yao yawe niyenye kudumu. Mistari ifuatayo inatilia mkazo jambo hili.

*Huninyua huninyua kichandani niyele*

*Hatutoki hatutoki mpaka tupigane kisi*

### **3.5.2 Kuhamasisha**

Kuna baadhi ya nyimbo za harusi za Waswahili ambazo hutekeleza jukumu la kuhamasisha wanajamii kuhusu wanafiki wanaoishi nao katika jamii. Katika jamii kuna watu ambao hujifanya marafiki wakawahadhaa wengine kwa lengo la kutaka kujua habari zao hasa zile ambazo ni za siri. Baada ya kuzifahamu, huanza kuzungumza habari hizo na watu wengine. Katika hali hiyo huwa hakuna siri tena. Waja huhamasishwa kuhusu watu kama hao ili wawe na tahadhari wakati wakizungumza na marafiki wao. Pia kuna nyimbo zinazohamasisha bwana majukumu yake

kama mlezi wa watoto wake na familia yake kwa jumla. Kuna haja ya kuhamasishwa ili apate kujua majukumu yake kwani yeye ndio mwanzo anaingia katika maisha ya ndoa.

### **3.5.3 Kuelimisha**

Nyimbo za harusi pia hutoa mafunzo kwa wanajamii waweze kujiepusha na baadhi ya matendo ambayo huenda yakawaletea balaa au majuto katika maisha. Wakati vijana wanajiingiza katika mapenzi ambayo matokeo yake ni ndoa, kuna haja ya kuelimishwa kwamba hali hiyo ya mapenzi wasiiweke sana moyoni kwani mambo hubadilika kadri wakati unavyoenda. Kupitia mafunzo watakayo yapata, watajitayarisha kwa kila jambo ambalo huenda likatokea katika maisha yao ya ndoa.

Kuna nyimbo zingine za harusi katika jamii ya Waswahili ambazo hutoa mafunzo kuhusu jinsi mwanamke anatakikana kuwa, kwamba mwanamke anatakikana kumsifu mumewe na sio kumkashifu au kuzungumza mambo mabaya kumhusu hata kama kuna ugomvi baina yao, mwanamke atakikana kuhifadhi ubaya wa mumewe kupitia kumsifu au kuzungumza mambo mazuri kumhusu.

### **3.5.4 Kukejeli**

Kuna baadhi ya nyimbo ambazo huhusisha wanawake kurushiana maneno ambayo mara nyingi huwa ni matusi na ya kuudhi. Tabia hii hupatikana katika jamii kwa kuwa wanawake ni watu wanaopenda kugombana kwa sababu ya vitabia vidogo vidogo miongoni mwao kama vile kupokonyana wapenzi, mabwana na kadhalika. Yule anayemchukua bwana wa mwenzake ndie humrushia maneno yule bibi kwa lengo la kumuudhi. Katika mstari huu unadhihirisha mambo haya. Mzuie mume,

*sikuja kumwita.*

### **3.5.5 Kuhifadhi Utamaduni**

Utamaduni hujumuisha mambo yote yanayofanywa na wanajamii katika jamii. Miongoni mwa mambo haya ni mapishi. Kunayo mapishi ya aina mbalimbali kutegemea na chakula kinachopikwa. Kuna baadhi ya nyimbo za harusi ambazo zinazungumzia kuhusu namna aina fulani ya chakula kinavyo tayarishwa, kupitia hali hii utaratibu wa kutayarisha chakula hicho unapitishwa kutoka kizazi hadi kingine. Kwa namna hii utamaduni wa jamii husika unahifadhiwa.

Kwa mfano kuna shairi kuhusu kipungu na jinsi anavyo tayarishwa kama kitoweo. Kupitia shairi hili ambalo hukaririwa wakati wa harusi, vizazi vijavyo vitafahamu jinsi ya kutayarisha kitoweo cha kipungu.

### **3.5.6 Kuzindua**

Hii ni hali ya kumfahamisha mtu kuhusu hatari au madhara ya jambo fulani ambalo huenda akawa analifaya lakini hafahamu matokeo yake. Kuna nyimbo za harusi katika jamii ya Waswahili ambazo zinazindua vijana kuhusu madhara ambayo huweza kumfika mtu kwa sababu ya kupenda.

Kupenda si kubaya lakini kuna haja ya kuangalia au kuchunguza, iwapo kupenda huko kutakuletea madhara basi hauna budi kukatisha mapenzi hayo, na iwapo kuna heri basi waweza kuendelea kupenda.

Mistari ifuatayo inadhihirisha kauli hii.

*Nimeenda digo, njia za hatari,*

*Si kucha milima, wala bahari*

*Moyo wakupenda, hauna nadhari*

### **3.6 Walengwa Wa Ujumbe**

Ujumbe unaojitokeza katika nyimbo za kiasili za harusi za Waswahili unalenga bwana harusi. Kuna zile zinazo muhamasisha kuhusu majukumu yake kama kiongozi katika familia. Ujumbe huu unapitishwa na wanaume ambao huwa wanacheza ngoma ya kiumbizi kumburudisha bwana arusi kabla ya sherehe yenyewe ya harusi.

Ujumbe mwingine wa bwana arusi hupitishwa na bibi akilalamikia jinsi pendo lao la awali alivyolibadili. Bibi anaendelea kumueleza jinsi alivyo mthamini kumbe mwenzake fikra na mawazo yake ni tofauti hata mwishowe anaowa mke mwengine na kugawa penzi hilo. Pia kuna nyimbo ambazo ujumbe wake unamlenga bibi. Ujumbe huu huwa unatoka kwa wanawake wengine ambao ni mahasimu wake kama vile mke mwenzau au hawara wa mumewe. Ujumbe huu huwa umejaa maneno ya vijembe ili apate kuudhika. Mbali na bwana na bibi kuna nyimbo ambazo ujumbe unalenga jamii kwa jumla. Kwa mfano kuna nyimbo ambazo bibi anampongeza mumewe. Lengo la bibi huwa yuataka waja wafahamu mazuri aliyonayo mumewe.

Pia kuna nyimbo ambazo hutoa habari kwa jumla kuhusu jamii ili wanajamii wapate kufahamu habari hizo. Hizi ni zile zinazoangazia au zungumzia tabia ambazo haziambatani na maadili ya jamii kama vile unafiki, uesharati na kadhalika.

### **3.7 Taarab**

Bendi ya taarab ni bendi ambayo mara nyingi hucheza katika sherehe za harusi za Waswahili na Wadigo. Bendi hii huchukuliwa kama kitumbuizo na kiburudisho katika pilkapilka ya sherehe hizi. Mara nyingi hucheza baada ya nikaha mchana na usiku pia. Sherehe huchukuliwa kuwa ni ya kufana iwapo watu waliohudhuria watatumbuizwa na bendi ya taarab, kwa sababu hii tumeona kunahaja ya kuchambua maudhui katika nyimbo zake. Mbali na

maudhui, tutaangalia majukumu yanayotekelezwa na nyimbo hizi pia tutaangazia walengwa wa ujumbe wa nyimbo hizi katika jamii.

### **3.7.1 Maudhui**

#### **3.7.1.1 Ukosefu wa imani**

Mwimbaji anasema katika wimbo wa Viumbe Wazito kwamba hawa watu ambao yeye amekuwa akiwachukulia kama watu muhimu sana kwake ndio ambao wamekuja kungeuka na kwamba wao sasa ndio wamekuwa watu wabaya sana na wasio na imani hasa kwa kile walichofanyiwa na mwimbaji. Mistari ifuatayo inaonyesha dhana hii ya ukosefu wa imani.

*Vile nilivyo wathamini nikawaekeni usoni.*

*Kumbe wakosefu wa imani*

*Hata hamna shukrani*

Mwanahawa Ali anaongeza kusema watu hawa hawana shukrani kwani yeye mwenye alikuwa amewathamini sana na pia kuwaweka usoni ama kuwapea kipao mbale kati ya anaowapenda lakini kumbe hawa watu wako tofauti na vile alivyowachukulia.

Mwanahawa pia anasema kwamba hawa watu wanamhiliki nakumtia ubayani, jambo ambalo yeye linamshangaza kwani amewafanyia hisani na haoni ubaya huo unatoka wapi.

#### **3.7.1.2 Kupeana tahadhari**

Katika wimbo huu wa Viumbe Wazito pia, Mwanahawa Ali anajaribu kupeana tahadhari kwa jamii kuhusiana na watu anaowazungumzia. Anaendelea kusema kwamba watu hawa ni wabaya sana kwani wao hawana jambo lolote ambalo watafanyiwa ambalo wao wataliona la maana. Mwanahawa anajaribu kuwapea tahadhari kwamba waendeleo na chuki, hila na mabaya

yote ambayo wanampangia lakini iko siku watajuta pengine kwa kupata adabu kutoka kwa Mungu Mistari ifuatayo inadhihirisha usemi huu.

*Nyie palilieni chuki, iko siku mtajuta*

### **3.7.1.3 Kutolipiza kisasi**

Mwimbaji anasema kwamba hata ijapo kuwa hawa watu wamemtendea mambo kinyume na yale yeye ameyatarajia kama shukrani kutoka kwa hawa watu baada ya kuwatendea mambo mazuri tu watu hawa wanamlipa kwa kumfanyia hila, kumsengenya na ubaya wote ule ambao unamfanya mwimbaji kushangaa kwa nini iwe hivyo.

Mbali na hayo yote ya kufanyiwa ubaya, Mwanahawa anasema kwamba yeye katu hata lipiza kisasi kwa ubaya anaofanyiwa. Mistari ifuatayo inadhihirisha kauli hii.

*Wala donge sitoweka*

*Muamini nina nia njeam kwenu nyie*

“Donge” hapo ni neno ambalo limetumiwa kuonyesha ama kumaanisha kisasi ambacho yeye anasema hawezi kuwawekea ama kulipiza kwani yeye ana nia njema kwao na kwamba yeye hatajenga uhasimu nao kwani hilo kwake ni sumu.

### **3.7.1.4 Masuala ya Dini**

Mwimbaji pia anajaribu kuleta swala la dini ndani ya wimbo huu wa Viumbe Wazito. Mwanahawa anasema kwamba yeye amewafanyia hawa watu mambo mengi mazuri lakini wao wanamtendea ubaya na pia hawana shukrani ila yeye anaimani kwamba utu wake hauwezi kuenda bure kwani Mungu yuko na ndiye tumaini lake kubwa. Mistari ifuatayo inadhihirisha usemi huu.

*Wema nimefanya hamna shukrani palipo bakia nashukuru Mungu.*

Mwimbaji anaimani kuwa Mungu atamlipizia kwa yote ambayo hawa watu wanamfanyia. Anashangaa kwamba hata baada ya kufanya wema kwa watu hawa, wao wanang'ang'ana tu kumchafulia jina ila yeye anaimani Mungu yuko muhukumu.

*Mola wetu naamini inshallah huku tutayatambua*

### **3.7.1.5 Uvumilivu**

Mwimbaji pia anajaribu kuleta dhana ya uvumilivu katika kila jambo ambalo mtu anapitia. Mwimbaji anasema hawezi kuutoa ubinadamu wake hata japo ni vigumu kwani yale anayotendewa ni vigumu kuvumilia.

*Sivui ubinadamu kwa mlonitendea*

Ingawaje ni vigumu kwa mja kuvumilia, ako tayari kuvumilia ijapo kwa mda mrefu lakini hayuko tayari kulipiza kisasi.

### **3.7.1.6 Malezi**

Mwimbaji anajaribu kutuambia kwamba yeye kama mzazi wa mwana, amejaribu kumlea mtoto wake tangu akiwa mtoto mchanga mpaka sasa amekuwa mkubwa na sasa amefikia umri wa kuolewa. Hii inadhihirisha dhana ya malezi kwani angekuwa hakumlea vilivyo ama katika mazingira mwafaka, basi hangeweza fikia kiwango kile cha kuweza kuolewa.

Mistari ifuatayo inadhihirisha dhana hii ya malezi.

*Nilipokulea mwanangu ulileleka*

*Leo ushapata wako mwanangu unaondoka leo*

Omar Kopa anajaribu kumwambia bintiye kwamba alimlea vizuri na katika mazingira mema kwa hivyo anatarajia amehitimu vyema kwenda kuanza jiko lake.



### 3.7.1.7 Mapenzi

Mwimbaji anajaribu kuonyesha dhana ya mapenzi katika wimbo wake, mwanzo kabisa anatuambia kwamba anadhania kwamba vile alivyomlea mtoto wake anamuona amekomaa vyakutosha kiasi cha kumruhusu aolewe.

Mistari ifuatayo inadhihirisha usemi huu:

*Boga ulilopenda mwanangu*

*Lipende na ua lake*

*Bwana uliyempenda mwanangu*

*Mpende na ndugu zake*

*Lolote likikushinda mwanangu uende kwa wazazi wake.*

Mwimbaji hapa anasisitiza dhana ya mapenzi ya kwamba ampende mumewe maana yeye mwenyewe kamchagua. Mbali na hilo, mwimbaji anasisitiza mwanawe akawapende ndugu na hata wazazi wa bwanake kwani haya yote ni ishara mwafaka ya mapenzi kwa bwanake na wale wote wenye kuhusiana na bwanake.

Omar anasisitiza dhana hii ya upendo na mapenzi pale ambapo anamwambia bibi arusi maneno yafuatayo.

*Mama kampende mume wako*

*Dada kampe mapenzi yako*

Hii ni ishara kamili ya mapenzi kama inavyojidhihirisha katika wimbo huu.

Katika mstari mwingine mwimbaji anasema,

*Mgawie visokwisha mkwe wangu*

*Mzidishe mudi*

Mwimbaji anamwambia mwanawe akamgawie mkwewe mambo matamu matamu na yasokwisha angalau aweze kumzidisha mori wa mapenzi mkwewe.

### **3.7.1.8 Maombi**

Mwimbaji anajaribu kuleta dhana ya maombi katika wimbo wake hasa pale ambapo anamuomba mwanawe safari njema na salama hasa pale mwanawe anaonekana yuko tayari kuenda kwa mumewe.

Omar anajaribu kuleta dhana hii kwa kutumia mistari ifuatayo katika wimbo.

*Nenda salamaa salama*

*Tutaonana tena Mungu akipenda kwa uwezo wa Allah utadumu naye huyo.*

Mistari hii inaonyesha dhahiri kwamba mwimbaji anamuomba dua njema mwanawe Mungu amlinde wakati yuko safarini na hata afikapo kwa bwanake bado anamuomba Mungu ndoa yao iweze kudumu.

Dhana ya maombi katika wimbo huu inajaribu kuwaunganisha watu na Muumba wao ambaye ndiye anayestahili kuombwa na kuabudiwa na mja yeyote yule.

### **3.7.1.9 Maadili katika ndoa**

Mwimbaji anajaribu kumwambia mwanawe kwamba wakati atakuwa katika ndoa yake azingatie mambo ambayo yatamfanya mumewe ampende na pia yeye mwenyewe ampende bwanake.

Anasisitiza kwa kumwambia kwamba katika ndoa, watu ambao hawataki kuwaona wakiwa pamoja watajaribu kwa kila njia na hila ili walipindue penzi lao hivyo yeye ajiepushe na vishawishi hivyo kwani vitamuacha avunje ndoa yake.

Mistari ifuatayo inaonyesha hali hii ya baba mzazi akijaribu kumrai mwanawe.

*Kuna videge viwili mwanangu*

*Vitakuja natishio*

*Vitajileta jileta kwa njia ya matamano.*

*Jua raha ya mapenzi mwanangu kalale na mumeo*

Omar kopa anaonyesha ni jinsi gani watu wanaweza kuingilia ndoa ya watu ili waivunje na ndio hapo anajaribu kumrai mwanawe ya kwamba ajieke tayari na vishawishi kama hivi ambavyo vyaweza kumvunjia ndoa yake.

### **3.8 Majukumu**

Nyimbo za taarab kama nyimbo nyingine zozote zile, zinatekeleza majukumu fulani. Majukumu haya huelekezwa kwa wanajamii ili waweze kuishi vyema katika jamii wanamoishi.

#### **3.8.1 Kuhimiza**

Baadhi ya nyimbo za taarab zinaanza kwa maombi au yanapatikana katikati ya wimbo. Hali hii inadhihirisha umuhimu wa kuelekea kwa Maulana kupitia kwa maombi katika shughuli yoyote unayofanya. Hata katika uhusiano wa kimapenzi, kuna haja ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu ili alinde uhusiano huo sije mahasidi wakaingilia na kuuvuja uhusiano huo.

#### **3.8.2 Huelimisha**

Nyimbo nyingi za taarab zinahusu mapenzi baina ya wapendanao. Nyimbo hizi zinaelimisha wanajamii hasa vijana ambao wanaingia katika maisha ya ndoa kuhusu maisha ya ndoa. Wakati msichana anapoolewa, kuna haja ya kuelezwa jinsi anavyotakikana kuishi na mumewe. Kwa mfano ampende, amuenzi na kadhalika.

Mbali na muwewe kuna wazazi na ndugu wa bwana, kuna haja pia ya kuwakubali na kuwapenda ili aishi vizuri katika boma la akina bwana.

### **3.8.3 Huzindua**

Nyimbo za taarab pia huzindua wanajamii kuhusu mambo yanayotendeka katika jamii. Katika jamii kuna watu ambao hawana shukrani kwa kila jambo jema wanalotendewa. Mbali na ukosefu wa shukurani, hawathamini jambo lolote linalofanywa na mwingine. Kuna haja ya wanajamii kufahamu kuwa watu kama hawa tunaishi nao na wasiwe kikwazo kwako cha kutotenda uadilifu kwa wengine.

### **3.8.4 Kukashifu**

Nyimbo za taarab zinakashifu baadhi ya tabia za wanajamii ambazo zinaenda kinyume na maadali ya jamii kama vile kusengenya, uvivu, wivu, usabasi na kadhalika. Vitendo hivi huleta madhara katika jamii kama vile kuvunjika kwa ndoa, ugomvi na kadhalika ndio maana hukashifiwa.

### **3.9 Walengwa**

Kwa kuwa ujumbe katika nyimbo za taarab huangazia matendo na tabia zinazodhihirika katika jamii kwa jumla, walengwa ni watu wote katika jamii. Mbali na maarusi na familia zao, ujumbe unakusudiwa kuwafikia pia wanajamii wengine ili wafahamu yale yanayotendeka katika jamii. Iwapo ni mazuri hawana budi kuiga na iwapo ni wabaya, wajiepushe nayo.

### **3.10 Kulingana Kimaudhui Baina Ya Nyimbo Za Kiasili Za Harusi Za Wadigo Na**

#### **Waswahili.**

Mbali na kwamba Wadigo na Waswahili ni jamii mbili tofauti ambazo huandaa sherehe zao za harusi tofauti, kuna mwingiliano wa kimaudhui baina ya nyimbo zao za kiasili zinazoimbwa kwa minajili ya kuburudisha waliohudhuria. Mbali na kuburudisha, huwa na ujumbe ambao nyimbo hizi hupitisha kwa wanaokusudiwa.

Katika jamii zote mbili, yaani Wadigo na Waswahili, nyimbo zao za harusi zinadhihirisha maudhui ya maombi. Wakati wowote wanapofanya jambo hutanguliza maombi kwa Mwenyezi Mungu kabla ya kutekeleza jambo hilo. Mbali na maombi kuna maudhui ya majukumu ya bwana katika familia. Jamii hizi mbili kila mojawapo iko na nyimbo ambazo zinaangazia kuhusu majukumu ya bwana katika nyumba.

Bwana ndiye mlezi yaani anastahili kukimu mahitaji ya familia yake. Kuna haja ya vijana kuhamasishwa kuhusu majukumu haya pindi waingiapo katika ndoa. Jambo hili hutekelezwa kupitia nyimbo ambazo huimbwa wakati wa sherehe za harusi.

### **3.11 Kutofautiana Kimaudhui Katika Nyimbo Za Asili Za Harusi Za Wadigo Na**

#### **Waswahili**

Licha ya mwingiliano uliopo baina ya jamii hizi mbili, ambao unasababishwa na ujirani, ndoa na dini ya kiislamu tofauti za kimaudhui zimeonekana katika nyimbo zao za harusi. Kuna maudhui ambayo yanadhihirika katika nyimbo za harusi za Wadigo lakini hayadhihiriki katika zile za Waswahili, pia kuna baadhi ya maudhui katika nyimbo za harusi za Waswahili ambayo hayapatikani kwa zile za Wadigo.

Maudhui yanayopatikana katika nyimbo za Wadigo pekee ni pamoja na umuhimu wa kuo mbali. Vijana katika jamii ya Wadigo wanahimizwa kuo au kuolewa mbali na kwao au katika jamii nyingine, ili kumwezesha kujua mengi kuhusu jamii hiyo.

Wazazi wa msichana huomba msamaha kutoka kwa jamaa ya mvulana kwa niaba ya familia ya msichana, na kutaka shughuli ya harusi itekelezwe bila kizuizi chochote.

Kunayo maudhui ya uvivu, ambayo huregelea tabia ya bibi arusi ya kutojishughulisha na kazi yoyote ya nyumbani ambapo kazi zote anamwacha mamavyaa kwa kuwa ni mvivu.

Mamake msichana wakati mwingine hukosa kuwajibika katika kumlea msichana wake ipasavyo.

Hushindwa kumfunza kazi za nyumbani kama vile kupika, kuosha vyombo na kadhalika.

Hali inayosababishwa na kuweco kwa mfanyikazi wa nyumbani.

Maudhui ya wivu ambayo yanajitokeza kupitia kwa bibi kwamba hafurahii mumewe akioa mke mwingine, hali inayomfanya afanye kila hila kuhakikisha kwamba bwanake haoi mke mwingine.

Ushirikina unadhihirika pale bibi anaenda kwa mganga kumfanyia dawa bwanake asiwe na nia ya kuoia mke mwingine.

Dhana ya umbeya inajitokeza katika nyimbo za harusi za Wadigo. Katika jamii ya Wadigo kuna baadhi ya watu ambao kazi yao ni kukaa vibarazani wakizungumza mambo yasiyowahusu na wasiokuwa na ushahidi nayo.

Kuna nyimbo ambazo huangazia tabia za baadhi ya wazazi katika jamii ambao huonyesha tamaa na ubinafsi wanapopewa pesa za kilemba na maziwa. Hali hii huwafanya kumpeleka bintiyao kwa bwanake pasi kumzawadi.

Kuna baadhi ya nyimbo ambazo huhimiza umoja na ushirikiano katika jamii ambao husababishwa na ndoa baina ya jamii mbili tofauti.

Maudhui yanayopatikana katika nyimbo za Waswahili pekee ni pamoja na mapenzi. Kuna nyimbo za harusi katika jamii ya Waswahili ambazo hudokeza mambo ya mapenzi. Katika nyimbo hizi huzungumzia kuhusu vitendo ambavyo hufanya penzi likadumu baina ya wapendanao.

Kuna baadhi ya nyimbo za harusi za Waswahili ambazo hudokeza kuhusu vitendo vya kuashiria tabia ya kinafiki.

Nyimbo zingine za harusi huwa zimejaa vijembe ndani yake. Vijembe hivi vinakusudiwa kumfikia bibi ambaye bwanake ana uhusiano na mwanamke mwingine.

Kuna nyimbo ambazo ni za kumsifu au kumpongeza bwana, na sifa hizi hutolewa na bibi yake. Sifa zenyewe zaweza kuhusiana na maumbile yake au kazi anayofanya.

Kuna nyimbo zinazodhihirisha maudhui ya majuto. Mara nyingi katika nyimbo hizi anayejuta huwa ni bibi. Hujuta kwa sababu ya tabia ya bwanake, ambayo hakuitarajia wakati wakioana.

Tabia hii ni kama vile uesharati au kuoia mke wa pili.

Pia kuna baadhi ya nyimbo ambazo zinaangazia kuhusu mapishi ya aina fulani ya chakula, jinsi ya kutayarisha chakula hicho na namna kinavyoandaliwa.

Kunazo nyimbo zinazodokeza kuhusu tabia ya uesharati kwamba wanawake wanagombana kwa sababu ya wanaume. Wakati mwingine ugomvi huu huwa ni baina ya mahawara wawili wa mwanamume mmoja au baina ya bibi na hawara wa bwanake.

Pia Waswahili wana nyimbo za harusi ambazo huangazia madhara ya kupenda. Wakati mwingine watu au mtu hufikwa na matatizo bila kujua kwa sababu ya kupenda kwamba wakati alipopenda hakuchukua tahadhari yoyote.

### **3.12 Ulinganishi wa kimajukumu baina ya nyimbo za kiasili za harusi za wadigo na waswahili.**

Nyimbo za harusi kama nyimbo zengine zile zinatekeleza majukumu mbalimbali katika jamii, mbali na kwamba Wadigo na Waswahili ni jamii mbili tofauti, majukumu yanayotekelezwa na nyimbo zao za harusi yanaulinganifu wa kiasi kikubwa.

Katika jamii zote mbili kuwa nyimbo zenye kutekeleza majukumu ya kuhifadhi mila na utamaduni wa jamii husika. Kuna baadhi ya utamaduni ambao ni muhimu kwa vizazi vijavyo katika jamii.

Utamaduni huu ni kama vile mapishi ambayo yanaangaziwa kupitia nyimbo katika jamii ya Waswahili nao Wadigo wanahifadhi mila ya kuanza safari kwa maombi.

Mbali na kuhifadhi, kuna nyimbo katika jamii hizi mbili ambazo hutekeleza jukumu la kuhimiza baadhi ya tabia katika jamii.

Kwa mfano, katika jamii ya Wadigo kuna wimbo unaohimiza vijana waoe mbali na kwao au katika jamii tofauti na yao.

Jamii ya Waswahili nao wana wimbo unaohimiza maombi na vitendo ambavyo hufanya ndoa ikadumu. Katika jamii zote mbili kuna nyimbo ambazo zinahamasisha kuhusu majukumu ya bwana katika familia. Vijana, wana haja ya kuhamasisha kuhusu majukumu haya kwa kuwa ndio mwanzo wanaingia katika majukumu hayo.

Mbali na mwingiliano wa kimajukumu tuliouona, bado kuna majukumu yanayopatikana katika nyimbo za harusi za Wadigo pekee na pia baadhi ya majukumu yanapatikana katika nyimbo za harusi za Waswahili na hayapatikani kwa zile za Wadigo.

Katika jamii ya Wadigo, kuna nyimbo za harusi zenye kutekeleza jukumu la kukashifu matendo ambayo hayaambatani na maadili ya jamii. Haya ni matendo kama vile uvivu, ushirikiana, umbeya, tamaa na ubinafsi. Matendo haya ni mabaya kwa kuwa huleta madhara katika jamii.

Katika Jamii ya Waswahili kuna baadhi ya nyimbo za harusi ambazo hutekeleza jukumu la kukejeli baadhi ya watu katika jamii kwa lengo la kuudhi watu hao kwa sababu moja au nyingine.



Mbali na nyimbo za kukejeli, Waswahili wana nyimbo za harusi za kuzindua wanajamii kuhusu madhara ambayo mtu hueza kumfika kwa sababu ya kupenda.

Hali hii hutokea pale mtu anampenda na kumuamini mtu ambaye hata hampendi bali anamfanyia mzaha tu.

Pia Waswahili wanazo nyimbo za harusi ambazo hutekeleza jukumu la kuelimisha vijana ambao wanaingia katika maisha ya ndoa. Kuna haja ya kuelimishwa kuhusu matendo ambayo yatafanya ndoa yao idumu.

Ulinganifu wa walengwa wa ujumbe baina ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili Walengwa wa ujumbe wa nyimbo za harusi katika jamii hizi mbili ni tofauti.

Katika nyimbo za Wadigo wanaolengwa na ujumbe wa nyimbo hizo ni maarusi na jamaa wao wa karibu, yaani bwana na bibi arusi na wazazi wao, baba na mama.

Ujumbe katika nyimbo za harusi za Waswahili unalenga bwana arusi na wanajamii kwa jumla.

### **3.13 Hitimisho**

Katika sura hii, tumejishughulisha na nyimbo za harusi za kiasili za Wadigo na Waswahili, pia tumeangazia zile za bendi ya taarab. Katika nyimbo hizi tumeangazia maudhui, majukumu na hadhira lengwa. Pia tumelinganisha na kutofautisha maudhui na majukumu baina ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili.

## **SURA YA NNE**

### **HITIMISHO**

#### 4.0 UTANGULIZI

Nia yetu katika sura hii ni kutoa muhtasari wa matukio ya utafiti wetu. Kutokana na matokeo ya utafiti wetu, tumeweza kujadili nadharia tete zetu pamoja na kuangazia matatizo ya utafiti wetu. Mwisho tumetoa mapendekezo ya tafiti za baadaye.

Muhtasari wa matokeo, lengo kuu la utafiti wetu lilihusu uchambuzi wa maudhui na majukumu yanayotekelezwa na nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Nyimbo hizi zinaangazia maswala mbalimbali yanayotendeka katika jamii. Ingawa utanzu wa nyimbo umeshughulikiwa na wahakiki wengi, swala la kulinganisha maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili halijashughulikiwa.

Sura ya kwanza ya utafiti, ilishughulikia utangulizi, tatizo, madhumuni, nadharia tete, sababu za kuchaguwa mada, upeo na mipaka, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti. Sura hii ilikuwa ndio msingi wa kazi yetu.

Katika sura ya pili, tumeshughulikia utaratibu wa harusi na ndoa za Wadigo. Katika utaratibu huu kuna kupeleka posa, kupeleka mizigo, matayarisho ya harusi na baadaye harusi yenyewe. Katika sura hii pia tumeshughulikia utaratibu wa harusi na ndoa za Waswahili. Katika utaratibu huu kuna kupeleka posa, kupeleka mahari na mwisho harusi.

Katika sura ya tatu, tulijikita katika uchambuzi wa maudhui na majukumu yanayojitokeza katika nyimbo za kiasili za harusi za Wadigo na Waswahili. Baada ya uchambuzi huu tulilinganisha na kutofautisha, pia tumechambua maudhui na majukumu katika nyimbo za bendi za harusi za Waswahili, mbali na maudhui na majukumu katika nyimbo hizi za harusi, tumeangazia hadhira inayolengwa na nyimbo hizi katika jamii. Nyimbo tulizokusanya kwa ajili ya utafiti huu ni za kiasili sita za Wadigo na sita za Waswahili. Mbali na hizi tumeteuwa mbili za bendi ya taarab.

#### **4.1 Upimaji Wa Madhumuni**

Utafiti huu umefanywa kwa madhumuni ya

1. Kuchambua maudhui na majukumu yanayotekelezwa na nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili.
2. Kulinganisha maudhui na majukumu katika nyimbo za harusi katika jamii hizi mbili, Wadigo na Waswahili.
3. Kubainisha walengwa wa ujumbe unaowasilishwa na nyimbo hizi za harusi.

Madhumuni haya yote yamebainishwa katika utafiti wetu, maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili yameainishwa kwa kuzingatia nyimbo zilizoteuliwa kwa ajili ya utafiti

Maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili yamelinganishwa. Tumegundua ya kwamba kuna maudhui yanayodhihirika katika nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Pia kuna tofauti ya kimaudhui katika nyimbo hizi, yaani kuna baadhi ya maudhui yanayopatikana katika nyimbo za harusi za Wadigo lakini hayapatikani katika nyimbo za harusi za Waswahili. Pia kuna baadhi ya maudhui yanayopatikana katika nyimbo za harusi za Waswahili lakini hayapatikani katika nyimbo za harusi za Wadigo.

Walengwa wa ujumbe unaowasilishwa katika nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili wamebainishwa, katika nyimbo za harusi za Wadigo wanaolengwa na ujumbe ni maarusi na jamaa wao wa karibu na wale wa nyimbo za harusi za Waswahili ni wanajamii wote.

#### **4.2 Upimaji Wa Nadharia Tete**

Tuliloshughulika katika utafiti huu ni uchambuzi linganishi wa maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Nadharia tete zetu zilikuwa tatu. Nadharia tete ya

kwanza ilihusu kauli kwamba kuna uhusiano mkuu kimaudhui kati ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili.

Hili limebainika kuwa ni kweli, kwamba uhusiano wa kimaudhui baina ya nyimbo za harusi za jamii hizi mbili ni mkuu.

Nadharia tete ya pili ni kuwa kuna uhusiano wa karibu wa majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na zile za Waswahili. Kulingana na utafiti tuliofanya kauli hii imedhihirika kuwa ukweli kwamba kuna uhusiano wa karibu wa kimajukumu baina ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Majukumu yanayotekelezwa na nyimbo hizi za jamii hizi mbili yana ulingano isipokuwa kuna majukumu mawili matatu yanayotofautiana katika jamii hizi.

Nadharia tete ya tatu ni kwamba hadhira inayokusudiwa katika nyimbo za harusi za Wadigo haitofautiani na ile ya nyimbo za harusi za Waswahili. Kauli hii si kweli kulingana na utafiti wetu. Matokeo ya utafiti wetu yanadhihirisha kwamba nyimbo za harusi za Wadigo, ujumbe wake unalenga maarusi na jamaa wao wa karibu na zile za Waswahili hadhira lengwa ni jamii kwa jumla.

#### **4.3 Changamoto Za Utafiti**

Kwa kuwa sampuli tuliotumia ni sampuli lengwa, kazi yetu ilikuwa na changamoto mbalimbali. Kwanza, nyimbo tulizozikusanya zilikuwa nyingi na za aina mbalimbali.

Ilitulazimu kuzichuja ili kupata sampuli tuliotumia katika utafiti wetu. Pili, ukosefu wa fedha za kuwezesha usafiri hadi sehemu ambayo ni chimbuko la data lilikuwa tatizo lingine. Mwisho, muda wa utafiti ulikuwa mfupi kuweza kupata habari zote zilizotakikana. Changamoto ambazo tumezitaja ni baadhi tu ya changamoto tulizokumbana nazo katika utafiti. Licha ya changamoto hizo tuliweza kukusanya data iliyotufaa katika utafiti wetu.

#### **4.4 Mapendekezo**

Utafiti huu ulihusu uchambuzi linganishi wa maudhui na majukumu ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili.

Tumegundua kuna uhusiano mkuu kimaudhui kati ya nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili. Pia tumegundua kwamba kuna uhusiano wa karibu wa kimajukumu baina ya nyimbo za harusi za Wadigo na zile za Waswahili. Tunapendekeza kuwa tafiti zingine zifanywe kuhusu ulinganishi wa fani katika nyimbo za harusi za Wadigo na Waswahili.

## MAREJELEO

- Askew, K. (1992) *Performing The Nation: Swahili Musical Performance and the Production of Tanzania National Culture*. Ph.D Thesis, Harvard University
- Beja, S.K. (2001) *Giriama Funeral Songs: Functional Aesthetic Study* Ph.D. Thesis, University of Nairobi.
- Fair, L. (2001) *Pastimes and Politics Culture, Community and Identity in Post-Abolition Urban Zanzibar, 1890-1945*: Ohio University Press.
- Indigasi, H. (1988) *Stylistics*. Nairobi: Nairobi University press.
- Khatib, M.S (1987) “*Taarab katika Fasihi Simulizi*” katika *Makala za Semina ya Fasihi, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. University of Dar-es-Salaam Pg. 16-25.
- Kingei, K. (1993) *Language Culture and Communication: The Role of Taarab Songs in Kenya 1963-1990*, Ph.D Thesis, Harvard University.
- \_\_\_\_\_ (1994) “*Swahili Taarab as a medium of Politics Expression in Kenya*” in *Writers Forum. A Journal of Fine Writers Association of Kenya* Vol. 2; Pgs. 74-91.
- Knappert, J. (1972) *A Choice of Flowers*. London: Heinmann
- Kuhenga, C. (1977) *Tamathali za Usemi*. Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau.
- Mazrui, A. and Shariff, I.N. (1994) *The Swahili Idiom and Identity of an African People*. Trenton: N.J Africa World Press.
- Mjomba, G. (2001), *Uchambuzi wa Nyimbo za Harusi za Wadawida, Tasnifu ya Uzamili*, Chuo kikuu cha Nairobi.
- Msokile (1993) *Misingi ya Uhakiki ya Fasihi*, Nairobi E.A.E.P
- Njogu, K. and Chimera R. (1990) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

- Njogu, K. na Wafula M. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Jome Kenyatta Foundation  
Nairobi
- Peter B. (1995) *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. London:  
Manchester University Press.
- Spear, T.T (1978), *The Kaya Complex*. Kenya Literature Bureau. Nairobi.
- Timammy (2002) *Mombasa Swahili Women's Wedding Songs: A Stylistic Analysis*, University  
of Nairobi. Haijachapishwa.
- Topp, J.F. (1992) *Women and Africanization of Taarab in Zanzibar*. PhD. Dissertation, London,  
London School of Oriental and African Studies.
- Trudgill, P. (1995) *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society* (3<sup>rd</sup> Edition),  
London: Penguin Books.
- Tuki (1981) *Kamusi ya Kiswahili*, Nairobi, Oxford University Press.
- Tuki (2000) *English-Swahili Dictionary*. Second Edition. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili  
Research.
- Veronica (2005), *Nafasi ya Mwanamke katika tenzi mbili ya Shabban Robert*. Utenzi Hati na  
Utenzi wa Hati wa Adili Mama. Nairobi University- Haijachapishwa.
- Wafula, R. M and Njogu, K. (2007) ; *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyatta  
Foundation.
- Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.  
\_\_\_\_\_ (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-  
Muwa Publishers.
- \_\_\_\_\_ (2002), *Uhakiki wa Fasihi*. Phoenix Publishers Ltd., Nairobi.

\_\_\_\_\_ (2003), *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Focus Publications Ltd.,  
Nairobi.

Yule G. (1996) *Pragmatics*. UK: Oxford University Press.



**KIAMBATANISHO I:**  
**BAADHI YA WAHOJIWA**

**Hassan Suleiman Kuchengwa**

Ni mzee mwenye umri wa miaka sitini. Amezaliwa Tiwi na anaishi pale amezaliwa. Alikuwa na mengi ya kutuambia kuhusu utaratibu wa harusi na ndoa katika jamii ya Wadigo. Alitueleza kwamba utaratibu huu huanza na kupeleka posa, kupeleka mizigo, matayarisho ya harusi na baadaye harusi na ndoa. Aliweze kutueleza haya yote kwa kuwa mbali na kushuhudia kwa majirani, amewaoza watoto wake wawili, msichana na mvulana.

**Halima Rama Sudi**

Ni mama mwenye umri wa takribani miaka hamsini hivi. Ni mzawa wa Msambweni lakini ameolewa Tiwi. Alisaidia katika kuainisha nyimbo za harusi za Wadigo kulingana na wakati ziinapoimbwa, kwa mfano wakati wa kupeleka mizigo na wakati wa sherehe ya harusi.

Mbali na kuainisha, alitueleza masuala yanayoangaziwa katika nyimbo hizi. Alinialika sherehe ya kupeleka mizigo na harusi ambazo zilifanyika Tiwi. Nilihudhuria sherehe hizo pamoja naye. Nilipata fursa ya kushuhudia nyimbo za harusi zikiimbwa katika sherehe hizo.

**Mwanamkuu Juma**

Ni mwanamke mwenye umri wa miaka hamsini. Ni mzawa wa Tiwi lakini ameolewa na anaishi Kombani. Yeye anashughulika na kuwaweka ndani wasichana waliochumbiwa yaani ni kungwi. Alitueleza jinsi anavyomuandaa msichana kwa maisha ya ndoa kabla ya harusi. Alitueleza kuhusu vyombo vinavyohitajika katika kikapu cha uchumba na begi. Pia alitueleza utaratibu wa

kupokea kikapu cha uchumba na begi. Alitueleza nyimbo zinazoimbwa na kuchambua vyombo vya kikapu cha uchumba na begi.

### **Thureya Ali Yusuf na Mariam Mjahidi**

Hawa ni wanawake wa makamo, takribani miaka arobaini hivi. Wamezaliwa Lamu. Walishirikiana katika kutueleza utaratibu wa ndoa na harusi katika jamii ya Waswahili wa Lamu. Walitueleza kwamba utaratibu huu unianza na kupeleka posa, kupeleka mahari na baadaye harusi na ndoa. Waliweza kutupatia utaratibu huu kufuatia shughuli za harusi walizo hudhuria, pia harusi zao walizo fanyiwa.

### **Fatma Lali**

Ni mwanamke wa umri wa miaka thelathini. Ni mzawa na mkaaji wa Lamu. Aliweza kutusaidia katika utafiti huu kwa kutukusanyia nyimbo za kiasili za harusi katika jamii ya Waswahili.

## **KIAMBATANISHO II:**

### **NYIMBO ZA HARUSI**

#### **NYIMBO ZA TAARAB**

##### **1. VIUMBE WAZITO**

*Vile nilivyo wathamini, nikawaakeni usoni,  
kumbe wakosefu waimani, hata hamna shukurani,  
vile nilivyo wathamini, nikawaakeni usoni  
kumbe wakosefu wa imani, hata hamna shukurani  
viumbe msiochukulika, viumbe wazito x2*

*Mlikusudia nini enyi wenzangu, wenzenu kunihiliki  
Mwanitia ubayani sihuilka yangumjue sifedheheki  
Mlikusudia nini enyi wenzangu mwenzenu kunihiliki  
Mwanitia ubayani sihuilka yangumjue sifedheheki  
Hamthamini hisani wala nguvu zangu viumbe hamchukuliki  
Nimeijenga imani thabiti moyo wangu kata sito taharuki  
Ninaamini hakika iko sku itafika tope mnazo npaka inje nitakasika x2*

*Wala donge sitoweka muamini mnania njema kwenu nyie x2*

*Sijui niwaweke fungu gani viumbe mhisabike x2  
Lafarasja kwenu dhiki jema kwenu baya  
Mwenzangu hamchukuliki ndivyo mliyvo zowea  
Lafaraja kwenu dhiki jema kwenu huwa baya  
Wenzangu hamchukuliki ndivyo mlivyo zowea*

*Mnanifuja kwa wote msonafadhili eti mna roho mbaya  
Mwanipigia epete kila mahala mbaya mimi mbaga.  
Mnanifuja kwa watu mso na fadhila eti mnaroho mbaya  
Mwanipigia upati kila mahala mbaya mimi  
Navumilia sikitu najuwa yenu hila mwenzangu nimezowea  
Mhukumu mola wetu naamini inshallah huko tutayatambua  
Navumilia sikitu najuwa yenu hila wenzangu mmezowea  
Mhukumu mola wetu naamini inshallah huko tutayatambua  
Wema wangu hauozi milele utabakia mfanyavyo roha radhi kinyongo sitowawekea x 2*

*Fadhilki mfadhili mbuzi binadamu ana maudhi kweli hiyo x 2*  
*Sijui niwaweke fungu gani viumbe muhisabike x 2*  
*Lafaraja kwenu dhiki jema kwenu huwa baya*  
*Wenzangu hamchukuliki ndivyo mlivyo zowea*  
*Lafara kwenu dhiki jema kwenu huwa baya*  
*Wenzangu hamchukuliki ndivyo mlivyo zowea.*

*Huu ubinadamu kwa mlionitendea ingawaje nivigumu kwa mja kuvumilia x 2*  
*Sitojenga uhasimu moyo umenitulia*  
*Kitu hicho kwangu sumu wala sitoupa njia sitojenga uhasimu, moyo umenilulia*  
*Kitu hicho kwangu nsunu wala sitoupa njia*  
*Nitawatendea wema mimi ninajali utu*  
*Wala sitorudi nyuma siwezi hilo kuntu*  
*Nitawatendea wema mininajali utu*  
*Wala sitorudi nyuma simzihito kuntu*

*Nipalilieni chuki iko siku mtajuta x 2*  
*Sijui niwaweke fungu gani viumbe muhisabike x 2*  
*Lafaraja kwenu dhiki jema kwenu huwa baya*  
*Wenzangu hamchukuliki ndivyo mlivyo zowea*  
*Lafara kwenu dhiki jema kwenu huwa baya*  
*Wenzangu hamchukuliki ndivyo mlivyo zowea.*

*Wema nimefanya hamna shukurani palipo bakia nashukuru mungu ee x 2*  
*Nilidhani wenzangu kumbe maadui zangu sasa nimerudi kwangu wanatabu walimwengu ee x2*  
*Tenda wema wende zako usingoje shukurani*  
*Sipoteze muda wangu pikenii genu majungu*  
*Wala sioni uchungu nimesafi moyo wangu*  
*Tenda wema wende zako usingoja shukurani*  
*Sipotezi muda wangu pikenii yenu majungu*  
*Wala sioni uchungu nimesafi mogo wangu*

*Wenenda nisaidie mama x 3*

## 2. NENDA SALAMA – OMAR KOPA

*Nilipokulea mwanangu ulileleka, leo ushapata wako mwanangu unaondoka x2*

*Nasema nilipokulea mwanangu ulileleka leo ushapata wako mwanangu unaondoka*

*Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka ee*

*Mama kaanze maisha yako mwanangu unaondoka ee*

*Mama kawatunze wakwezako mwanangu unaondoka ee*

*Mama kampende mume wako mwanangu umeeondoka ee*

*Boga ulilopenda mwanangu lipenda na uwa lake*

*Bwana uliyependa mwanangu mpende na ndugu zake*

*Lolote likikushinda mwanangu uende kwa wazazi wake*

*Nilipokulea mwanangu ulileleka leo ushapata wako mwanangu unaondoka ee*

*Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka ee*

*Dada yaanze maisha yako mwanangu unaondoka ee*

*Mama kampende mume wako mwanangu unaondoka ee*

*Dada kampe mapenzi yako mwanangu unaondoka ee*

*Haya yote ni maisha mwanangu nawewe kajitahidi,*

*Yasije kibabaisha mwanangu kucheka hana budi*

*Majani viso kwisha mkwa wangu mzidishe mudi*

*Nilipokulea mwanangu ulileleka leo mumpata wako mwanangu unaondoka ee*

*Nasema yote ni maisha nawe mwanangu kajitahidi, yasije kubabaisha*

*Mwanangu kucheka huna budi, mjawe viso kwisha mkwewangu mzidishe mdadi.*

*Nilipokulea mwanangu ulileleka, leo umepata wako mwanangu unaondoka ee*

*Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka ee*

*Mama kaanze maisha yako mwanangu unaondoka ee*

*Mama kawapende bakwezako mwanangu unaondoka ee*

*Mama kampende mumuwako mwanangu unaondoka ee*

*Kuna videge viwili mwanangu vitakuja na tishio vitajileta jileta kwa njia ya matamano jua raha ya mapenzi mwanangu kalale na mumeo.*

*Nilipokulea mwanangu ulileleka leo umepata wako mwanangu unaondoka ee*

*Nasema kuna ndege wawili mwanangu watakuja na tisho, watakufuata kufuata kwa njia ya matamano jua raha ya mapenzi mwanangu wale na mumeo.*

*Nilipokulea mwanangu ulileleka leo umepata wako mwanangu unaondoka ee*

*Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka ee  
Mama kaanze maisha yako mwanangu unaondoka ee  
Mama kampende mume wako mwanangu umeondoka ee  
Mama utunze heshima yako mwanangu unaondoka ee  
Mama leo umepata wako mwanangu umeondoka ee  
Mama kampende mume wako mwanangu unaondoka ee*

*Nenda salamaaa salamaa nenda salamaa salamaa  
Nenda salamaa mwanangu salama nenda salama salamaa  
Tutaonana tena mungu akipenda nenda samaamaa salaa  
Kwa uwezo wa Allah utadumu naye huyu, nenda salaama salaa  
Nenda salaamaa salaamaa nenda salaamaa salaamaa*

*Kweupe kule pwani kweupe kuna madege  
Kweupe kule pwana kweupe kuna madoa  
Kweupe kule pwana kweupe kuna madoa  
Kweupe kule pwana kweupe kuna madoa  
Kweupe kule pwani kweupe kuna madege  
Kweupe kule pwana kweupe kuna madoa  
Kweupe pwani kweupe kuna njiwa weupe  
Kweupe kule pwana kweupe kuna madoa meupe  
Nenda salaama salaama nenda salaamaa salaama  
Nenda salaama mwanangu salaamaa nenda salaama salaamaa*

*Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka ee  
Mama kaangaze maisha yako mwanangu waondoka ee  
Mama kampende mume wako mwanangu unaondoka ee  
Mama utunze heshima yako mwanangu unaondoka ee  
Mama leo umepata wako mwanangu unaondoka ee  
Mama kaanze maisha yako mwanangu unaondoka ee  
Mama kampende mume wako mwanangu unaondoka ee  
Mama utunze heshima yako mwanangu unaondokae.*

## **NYIMBO ZA KIASILI ZA WADIGO**

### **1) Salama**

*Salama wee navyoya salama*

*Salama x 2*

*Kulola kure ni kumanya siri za atuu*

*Siri za atuu zinahadza kaya ino chivyere anamba*

*Samahani wee navoya*

*Salama salama*

*Salama wee ukaowe salama*

*Salama x 2*

*Salama wee uye salama*

*Salama x 2*

### **Tafsiri**

Salama anaomba sala

Ukiowa mbali utajua siri za watu.

Siri za watu zinataja mji huu

Chivyere anasema

Samahani naomba salama salama

Salama ukaowe salama

Salama

Salama turudi salama

Salama

### **2. Chivyere**

*Chivyere waniphani myao*

*Waniphani myao*

*Wanipha maphephe x 2*

*Kuni niphiye mwenye*

*Mkazamwana anarora*

*Madzini niphiye mwenye*

*Mkazamwana anarora*

*Vyombo nisuwe mwenye*

*Mkazamwana anarora*

*Kuphera ni phyere mwenye*

*Mkazamwana anarora*

*Kubiya niye mwenye*

*Mkazamwana anarora*

*Chivyere waniphani myao*

*Tabu nicherenayo*

**Tafsiri**

Chivyere ulinipa nini mwenzio  
Ulinipa nini mwenzio  
Ulinipa maganda x 2  
Kunini niende mwenyewe  
Mkazamwana anangalia  
Maji nikateke mwenyewe  
Mkazamwana anangalia  
Vyombo nioshe mwenyewe  
Mkazamwana anangalia  
Vyombo nioshe mwenyewe  
Mkazamwana anangalia  
Kufagia nifagie mwenyewe  
Mkazamwana anangalia  
Kupika nipike mwenyewe  
Mkazamwana anangalia  
Chivyere ulinipa nini mwenzio  
Tabu bado nikonayo

**3. Barua**

*Nasomerwe baruwaye rero*  
*Naisomwe x 2*  
*Bwana arusi asomerwe baruwaye*  
*Namupha mwana*  
*Mwana ni barubaru*  
*Usimuphe tenge wala usiphuphe gushe*  
*Mukatire lesa nasiliki wee*  
*Mwenye abwambwarise*

**Tafsiri**

Nasomewe barua yake leo naisomwe  
Bwana arusi asomewe barua yake  
Nampa mtoto  
Mtoto ni kijana  
Usimnunulie tenge wala kaniki  
Mnunulie lesa na siliki  
Mwenyewe aringe.



#### **4. Kunde**

*Kundee mbwago*  
*Ziriche ziokohe x 2*  
*Kundengwa za mayo ziriche ziokohe*  
*Kundengwa za wawa*  
*Ziriche ziokohe*  
*Bwa bwa bwa*  
*Ziriche ziokohe x 2*  
*Avimwamba mnarora*  
*Rorani vinono*  
*Msibanange kaya yehu na umbeya*  
*Mwi mrorwao mnavibako*  
*Mharusi mzima*  
*Wagwirwa na kuku mwiru*  
*Aya lagulwa*  
*Gwinyo gwinyo*  
*Anaphiha muzukani*  
*Akaloge mlumeye mweye asihale mchetu wa phiri*  
*Shaidi ni wawaye*

#### **Tafsiri**

Kunde mbwago, ziache zitokote  
Kunde za mama, ziache zitokote  
Kunde za nyaya, ziache zitokote  
Bwabwabwa  
Ziache zitokote  
Kama ambaye mlisema mnaowa, oweni vizuri  
Msiharibu mji wetu na umbeya  
Nyinyi mnao olewa ni wachokozi  
Bibi arusi mzima, alishikwa na kuku mweusi  
Anaenda kutibiwa , gwinyo gwinyo  
Anaenda kwenye mizimu  
Akamroge bwanake, asiowe mke wa pili  
Shahidi ni nyanyake.

#### **5. Sheria**

*Sheria wee sheria*  
*Chivyere mwayangu anawaibu*  
*Sheria muondo ligunzu x 2*  
*Sheria muondo ligunzu*  
*Mayo wee kuna baba kassim*  
*Wagwira maganage*  
*Achika mfukoni*  
*Mwari kayafungulwa*  
*Kumanina*  
*Chivyere mwayangu anawaibu sheria muondo ligunzu.*

**Tafsiri**

*Sheria wee sheria  
Chivyere wenzangu anaibu  
Sheria ni kesho asubuhi  
Sheria ni kesho asubuhi  
Mama yangu kuna baba kassim  
Alichukua mamia yake akaeka mfukoni  
Bibi arusi hakupewa zawadi  
Chivyere wenzangu anaibu  
Sheria ni kesho asubuhi.*

**6. Mduruma na mdigo,**

*Mduruma na mdigo, rero andagwirana x 2  
Rero andagwiranaa, Mayo wee naphiha  
Golini nikalole mwanangwa  
Anangwa ahenda vyalika  
Chivyere wee unaphaya phaya  
Mduruma na mdigo, rero andagwirana*

**Tafsiri**

Mduruma na mdigo, leo watashikana  
Leo watashikana  
Mama yangu naenda, golini nikaowe mtoto wa wenyewe  
Watoto wa wenyewe waliza likana  
Chivyere wewe unamchezo  
Mduruma na mdigo, leo watashikana

## NYIMBO ZA KIASILI ZA WASWAHILI

### 1. Randa

*Chacha rigombo  
Kwerekweche Mwana Ware!  
Kwa Nzee Madi Shee,  
Karibuni tunwe mayi  
Ndo tuteze ngoma,  
nataka unielezee  
tuiye tuteze ngoma  
kuiumbuka zamani,  
tuiye kuteza ngoma*

*Ya Rabbi,takabalie dua  
Kuikumbuka zamani,  
Tuiye kuteza ngoma*

*Kesho tapiga shindo  
Asanti Madi Shee*

*Kuoweya ni kazi yake*

*Tuiye kwa Madi Shee,  
Kumsaidii kuteza  
Kumsaidi kuteza,  
Tuiye kwa Madi Shee  
(Zigelegele)*

*Tuiye kwa Madi Shee  
Kumsaidia kuteza  
Kumsaidia kuteza,  
Tuiye kwa Madi Shee  
Mja hawezi kupanda,  
Hawezi kufunga mvua  
Hawezi kufunga mvua,  
Mja hawezi kupanda*

*Rigombo,Rigombo,Rigombo  
Chacha Rigombo  
Kwerekweche mwanaware*

## **2. Vugo**

*Lulu muenda chombo kakiteremsha pwani x2  
Kaitia mwanaudha na mabaharia ndani  
Kama mvuvi wa pweza tutakutana mwambani*

*La waridi la waridi hufumba likifumbua x2  
Na harufu na harufu imenijaa kifua  
Ukombali ukombali kikupenda kutojua*

*Yomi mami yomi mame huba huniteza shere x2  
Huninyua huninyua kichandani niyele  
Piga kusi piga kusi mwenye kujera ajere*

*Dunduu dunduu sinigongee dirisha x2  
Bwana hako bwana hako wendee kuswali Isha  
Si wajibu si wajibu mgeni kukaribishwa*

*Sikuveko sikuveko chungu chikichekechea x2  
Valoweka valoweka validhidi kutotea  
Mwanamume ni mtuzi kila mtu huchovea*

*Bosi langu bosu langu hufanya kazi ofisi x2  
Mwendo wake mwendo wake huenda kama tausi  
Hatutoki hatutoki mpaka tupigane kisi*

## **3. Kiumbizi**

*Kufa kupona  
Kiumbizi ngoma*

*Wanao walia ndege  
Wee leo mwandege  
Wanao walia  
Ukenda phwani  
Wania kuwia  
Wanao walia*

*Ulee ulele na ulele ngoma  
Ndio mema  
Nakunwa maji ya nt<sup>h</sup>o p<sup>h</sup>anga  
Ndio mema*

*Nende nayo  
Rudi nayo  
Leo maji yakijara  
Niwe membe  
Niwie nayo*

*laliwa haliwa  
Haliwa kijongoo haliwa*

*Banja kijinu banja  
Hodi nsumizeni kaya hodi  
Ntarnbale nao  
Ulimwengu sina maisha nao*

*Pwani kuna ua  
Lyalengwa gema  
Yalia wee  
Ng'ombe baa*

*Twende Jumbe ukaole  
Uchezavyo nnemo*

*Jambo haliwa  
Ukita nsimamizi  
Na majaaliwa*

#### **4. Kipungu**

*Kwa raha iso kiasi, ilio moyoni mwangu.  
Nipeni wino mweusi, niwasifie “kipungu”.  
Kwa uzuriwe halisi, mtamu aso tewengu.  
Kipungu jama kipungu.*

*Ninamsifu kwa wema, mumtambuwe vizuri.  
Mwanzo mpate na sima, alafu na kachumbari.  
Ni tamu isiokoma, kwa matonge furifuri.  
Kipungu jama kipungu*

*Nikikupa la zaidi, umtiye kwa mtuzi.  
Hakika utafaidi, haswa ukiwa wa nazi  
Vile utavyoburudi, chungu sijambe mashuzi.  
Kipungu jama kipungu.*

*Pili kwa harufu yake, ninakupa la ukweli.  
Jamani huwa kivyake, waeza ilia wali.  
Tena ule na ulike, hata waeza ilia wali.  
Kipungu jama kipungu.*

*Tammati muishilio, mwisho hapa napadara  
Jama nawambia leo, mujuwe lenye busara.  
Tukija kwa vitoweo, kwangu kipungu ni bora  
Kipungu jam kipungu.*

## **5. Uchekeche**

*Uchekeche mkono ee hae x 2*

*Ulie wali barrio hae uchekechee mkono*

1) *Haya hunipacha imi hee hae  
Mwenye haya na huruma  
Kwingi kusimama nayo ee hae  
Siwezi kuyasukuma  
Shirika halina wema eee hae  
Na mla pweke hakuna.*

2) *Kikumbuka duniya eee hae  
Ruhu huniambia lia  
Wala hakuna rafiki ee hae  
Wakusafiana nia  
Hawa ndiyo kina panya ee hae  
Huuu wakivuzia*

3) *Sinitie mahabani eee hae  
Imi kwangu yagurie  
Wala hayadirikani eee hae  
Na huruma ni kasie  
Aloondoa hisani ee hae  
Udhulumie iye.*

## **6. Pendo**

*Alahu ya rabba, ilahi wahida,  
Nipe malilaba, yusipite muda,  
Iwe saajaba, uniepue shida,*

*Nilikupenda, pendo la imani  
Nikikufanya wanda, kukutia machoni,  
Kumbe ni samba, hunilaza ndani,*

*Pendo la wawali, la zama za tangu,  
Hakika umelibadili, liko kwa mwenzangu,  
Kwa hivyo himili, farikano langu*

*Yaa laitani, nilifahamu awali,  
Ndani moyoni, nisingekuweka asili,  
Kwani hufaeni, moyo si ramli,*

*Nilisalilika, nilikitambua,  
Nikauisha kumbura, sikuweza kuvaa,  
Kwa mwenye subira, mahaba kukaa,*

*Haya niliyoyaanza, leo nayahitimisha  
Japo nakupenda, nitajikazanisha  
Mimi na wewe nyonda, basi llumekwisha.*

*Nimeenda digo, njia za hatari,  
Si kucha milima, wala bahri,  
Moyo wakupenda, hauna nadhari.*

*Mzuie mumeo, sikuja kumwita,  
Sikufanya tanzi, kaja kamkota,  
Alipiga hodi, kamwambia pita,*

*Siwa hapa, na kijanae ni majeni  
Jina lake hapa, simlai asilani,  
Kuna chui hapa, mepokwa nyawa kinijwani*

*Hakupokwa chui, na nyama kinywani  
Bali amekula chui, firigisi na maini,  
Amewaachia mifupa, mashundrwa gaguneni,*

*Kunejuni na chawa, wote ni dhalimu,  
Kazi yao hula, ya uiumbe damu,  
Hucha kuwawa, mbona hula sumu*

*Kuna duko waungwana, wamawili masikio  
Alimsikia akinena, bubu matamko hayo,  
Naye kipofu alimuona, kiwehe kienda mbio.*

*Mwanangu kenyewa, usimfuate kozi,  
Ungali mjinga, hajajua kazi,  
Muhogo jiweni, haushushi mzizi,*

*Sitaki kuwa simaku, niyararue majabai,  
Kwa kila aliyehasidi, kwa macho asinione  
Sindano huwa na uzi, na kushona isishone,*

*Kuna malusha na tui, kujua ni udamisi,  
Mataza ni mwende ui, ni kitu kilo kipesi,  
Mwenye macho hafungui, punde humwita farasi,*

*Mwenda mbio sakafuni, sijiudhi kumwandama,  
Walio lala amkeni, msiji tweke zahama,  
Hakuna raha chuoni, mwanaharamu wa mama,*

*Zamani za leo, ni zamani gani,  
Umswafiyeo, nakumwamini ,  
Ndiye akuumao, na kulalandani,*

*Zamani zilizo pita, niilikuwa mtumwa wako,  
Ulitakalo nikifuata, kutii amri zako,  
Sikuona nilopata, ndipo kaondoka kwako,*

*Sichezi kerewa , na nngoma za kusi,  
Sivunji maruwa, kwa shavu la nsi,  
Asiye nitambua, na mimi simuisi,*

*Twin na ratwabu, ziembetwe na chaka,  
Hazina sharabu, majini hupuputuka,  
Ulioniharibu, niniu wewe kumbuka,*

*Kisu kimekoma maso, ila zijaya huchinja,  
Niacheni ni nyamaze, nisiamshe wajinga,  
Paka ameiba samaki, ndani majini yuwaenda*